# Nipashe JUMAPILI

Jumapili Novemba 15, 2020 • Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

MWANGA WA JAMII

ISSN 0856 • No. 0580400

www.ippmedia.com

www.twitter.com/nipashetz

www.facebook.com/nipashetz

www.instagram.com/theguardian_newspaper

LIKE & FOLLOW US


**BABU** aanzisha darasa kufundisha vijana Kiingereza

UKURASA 5



**VIONGOZI,** wafuasi CHADEMA wazidi kuhenya rumande

UKURASA 2




UKURASA 9

RIPOTI MAALUM

# Utupaji taka unavyoweka rehani Hifadhi ya Mikumi

**KILA** siku zaokotwa kilo 300, nyani wabadili mlo... *Endelea Ukurasa wa 4*



## Mabilioni yanaswa malipo hewa ujenzi wa stendi ya mabasi Dar

UKURASA 2

Mkurugenzi Mkuu wa Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU), Brigedia Jenerali John Mbungo, akionyesha zaidi ya Sh. milioni 100, zilizookolewa na taasisi hiyo, baada ya kuchepushwa kwa njia ya udanganyifu kutoka shirika la kimataifa lisilo la kiserikali, zilizokuwa zielekezwe kwenye huduma za afya jana. Kulia ni Mkuu wa Ukaguzi wa Ndani wa shirika hilo, Rehema Mkumbwa. **PICHA: JUMANNE JUMAN**

## Nyumba ya DED yateketea kwa moto

UKURASA 2'




Scan Hapa

Fungua App ya QR Code Reader kisha scan kupakua APP yetu

Google Play App Store


MICHEZO **STARS YAJIPANGA 'KUPINDUA MEZA'** UK.24

**MAONI, KATUNI** UK.6

HABARI KITAIFA

## Nyumba ya DED yateketea moto

**Na Richard Makore,** SIMIYU

NYUMBA ya Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Meatu, mkoani Simiyu, imeungua kwa moto usiku wa kuamkia jana.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Simiyu, Kamishna Msaidizi (ACP), Richard Abwao, alikiri nyumba hiyo ya Fabian Manoza ambaye ni Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri hiyo, kuungua moto na kwamba chanzo chake ni hitilafu ya umeme.

Alisema kwenye nyumba hiyo, alikuwapo mdogo wa mkurugenzi hiyo ambaye aliona moshi ndani.

Pia alisema kutokana na moshi huo mtungi wa gesi ulilipuka ndipo alipotoa taarifa polisi.

Kamanda Abwao alisema baada ya kupata taarifa hizo, askari polisi walifika na kuokoa gari lililokuwa jirani na nyumba hiyo na kwamba walichukua uamuzi wa kuvunja kioo ili kuondoa 'handbrake' ya gari na kuliondoa.

Abwao alisema polisi bado wanaendelea na uchunguzi na kwamba mali zote zilizokuwa ndani ziliteketea.

Alisema Jeshi la Zimamoto na Uokoaji pamoja na Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO) walifika eneo hilo na kwamba kwa sasa ni mapema kuhusisha tukio hilo na jambo lolote.



Katibu Mkuu Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, Balozi Brigedia Jenerali Wilbert Ibuge (kulia), akizungumza na Balozi wa China nchini Wang Ke (katikati), walipokutana ofisini kwake jijini Dodoma jana. **PICHA: WIZARA YA MAMBO YA NJE**

# Mabilioni yaokolewa malipo hewa ya ujenzi wa stendi Dar

**Na Beatrice Shayo**

TAASISI ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU), imeokoa Sh. bilioni 12 zilizokuwa mbioni kutumika kwa malipo hewa ya ujenzi wa stendi mpya ya mabasi Mbezi, jijini Dar es Salaam.

Mkurugenzi Mkuu wa TAKUKURU, Brigedia Jenerali John Mbungo, alibainisha kuwapo kwa dosari hiyo alipozungumza na waandishi wa habari jijini Dar es Salaam jana.

Alisema fedha hizo zilikuwa mbioni kulipwa kwa wakandarasi kama ziada kwa kazi ambayo haikufanyika katika ujenzi wa stendi hiyo mpya ya mabasi.

"Kama ambavyo mlisikia Mheshimiwa Rais akizungumza wakati akizindua ujenzi wa stendi hiyo mpya ya mabasi hivi karibuni pale Mbezi, aliagiza kuhakikisha hakuna fedha ya serikali ambayo inafanyiwa ubadhirifu," alikumbusha.

Kiongozi huyo wa TAKUKURU aliendelea kubainisha kuwa: "Tunapenda kuufahamisha umma kwamba TAKUKURU kwa kushirikiana na Mkurugenzi wa Jiji la Dar es Salaam, Zipora Liana, tumekuwa tukifuatilia utekelezaji wa mradi huu na mpaka sasa tumefanikiwa kudhibiti zaidi ya Sh. bilioni 12 ambazo zingeweza kulipwa kwa wakandarasi kama ziada kwa kazi ambayo haikufanyika."

Alisema udhibiti huo umefanikiwa kwa kuwa wachunguzi na wataalamu wa ujenzi kutoka TAKUKURU wamekuwa wakifuatilia kazi hiyo kwa karibu.

Brigedia Jenerali Mbungo pia alibainisha kuwapo kwa mahojiano yanayoendelea kuhusu suala hilo, hivyo asingependa kuwataja wahusika kwa kuwa kuna ambao wapo mtaani hawajakamatwa.

Vilevile, alikabidhi Sh. milioni 118.23 kwa mwakilishi wa Shirika la Kimataifa Lisilo la Kiserikali, zilizokuwa zimechepushwa kwa njia ya udanganyifu.

Alisema fedha hizo ni sehemu ya Sh. milioni 300 zilizotolewa na mfadhili kwa ajili ya huduma za afya nchini, lakini zikachepushwa.

"Kutokana na uchunguzi wa TAKUKURU, jumla ya fedha ambazo zimerejeshwa na watuhumiwa mpaka sasa ni Sh. 118,230,600 (milioni 118.23) ambazo leo (jana) hii tumezikabidhi kwa mwakilishi huyu," alisema.

Mbungo alisema kiasi cha Sh. milioni 172 ambazo zimebaki, zitarejeshwa ndani ya miezi mitatu kuanzia sasa hadi kufikia Januari mwakani.

Alitoa wito kwa mashirika mengine yasiyo ya kiserikali, kupeleka taarifa kama wanavyofanya shirika hilo ili wahusika katika ubadhirifu wachukuliwe hatua stahiki.

# Viongozi CHADEMA wazidi kusota rumande

**Na Elisante John,** SINGIDA,

VIONGOZI na wanachama 20 wa Chama Cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA), wataendelea kukaa mahabusu hadi keshokutwa baada ya kesi inayowakabili kuahirishwa.

Keshi hiyo ilitajwa juzi katika Mahakama ya Hakimu Mkazi Mkoa wa Singida na kusababisha mvutano mkali baina ya mawakili wa serikali na Emmanuel Makiya kutoka Arusha, anayewatetea washtakiwa hao.

Viongozi na wanachama hao, wakiongozwa na Mwenyekiti wa Mkoa, Emmanuel Jingu, walifikishwa mahakamani hapo kwa mara ya kwanza Novemba 2, mwaka huu, kwa mashtaka matatu likiwamo la kuendesha genge la uhalifu, ambalo halina dhamana.

Mwanasheria wa Serikali, Michael Ng'hoboko, alidai mahakamani hapo mbele ya Hakimu Mkazi Mfawidhi Consolata Singano kuwa kutokana na mashtaka wanayokabiliwa nayo, dhamana iko wazi kwa masharti ya Sh. milioni 10.

Hata hivyo, alidai kuwa Mahakama ya Hakimu Mkazi haina mamlaka ya kutoa dhamana isipokuwa Mahakama Kuu.

Wakili Makiya kutoka kampuni ya mawakili ya Mhyellah and Advocates ya mkoani Arusha, alipinga hoja hiyo kwa madai kuwa mahakama hiyo ina uwezo wa kutoa dhamana, hali iliyomlazimu Hakimu Singano kuahirisha kesi hiyo hadi Jumanne ijayo, atakapotoa uamuzi wa kutoa dhamana au la.

Kutokana na kuahirishwa kwa kesi hiyo, nje ya mahakama, ndugu, jamaa na marafiki waliangua kilio kutokana na washtakiwa kurejeshwa mahabusu.

Washtakiwa kwa pamoja wanadaiwa kufanya kosa hilo Oktoba 29 na Novemba Mosi, mwaka huu, katika mtaa wa Minga, barabara kuu ya Arusha

Mbali na kudaiwa kuendesha genge la uhalifu, pia wanadaiwa kula njama kwa nia ya kutenda kosa la uhalifu na kufanya mkusanyiko usio halali, hali inayohatarisha usalama wa nchi. Washtakiwa wote wamekana tuhuma hizo.

HABARI KITAIFA

## Bandari Dar kinara kwa ubora Afrika

**Na Elizabeth Zaya**

BANDARI ya Dar es Salaam imechaguliwa kushika nafasi ya kwanza katika bandari bora Afrika.

Bandari hiyo imeshika nafasi hiyo kwa mara ya kwanza na kuzishinda Port Elizabeth ya Afrika Kusini ambayo imeshika nafasi ya pili na Cape Town pia ya nchini humo iliyoshika nafasi ya tatu.

Zingine zilizoshika chati ya ubora ni Durban pia Afrika Kusini iliyoshika namba nne, Mombasa ya Kenya ambayo imeshika nafasi ya tano na Zanzibar, nafasi ya sita.

Ripoti hiyo ni kwa mujibu wa World Travel Awards (WTA) iliyotolewa Novemba 11, mwaka huu ambayo imekuwa ikitoa ripoti kwa sekta zinazotoa huduma za uchukuzi duniani.

Katika ripoti iliyotolewa mwaka jana na shirika hilo, Bandari ya Dar es Salaam ilishika nafasi ya nne katika bandari bora Afrika, huku nafasi ya kwanza ikishikwa na Durban ikifuatiwa na Port Elizabeth na Cape Town huku ya tano ikiwa Mombasa.

Mwaka 2018, Dar es Salaam ilishika nafasi hiyo ya nne, huku nafasi ya kwanza ikishikwa na Durban, nafasi ya pili Port Elizabeth, ya tatu Cape huku Mombasa ikishika nafasi ya tano.

# Aliyesakwa na TAKUKURU miaka minne ajisalimisha

**Na Beatrice Shayo**

MFANYABIASHARA aliyekuwa anatafutwa na Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) kwa kipindi cha miaka minne akituhumiwa kuwatapeli wananchi Sh. milioni 42, amejisalimisha ili kurejesha fedha hizo.

Mkurugenzi Mkuu wa TAKUKURU, Brigedia Jenerali John Mbungo, alibainisha hayo jana jijini Dar es Salaam alipozungumza na waandishi wa habari kuhusu hatua mbalimbali zinazochukuliwa na ofisi yake katika kuongoza mapambano ya rushwa.

Alisema tangu mwaka 2016, walikuwa wanamtafuta mfanyabiashara huyo kutokana na kudaiwa kufanya udanganyifu wa fedha za wananchi katika Mkoa wa Manyara.

Alisema TAKUKURU Mkoa wa Manyara wamefanya uchunguzi kwa dhuluma iliyofanyika kwa wajasiriamali 300 kutoka Wilaya ya Hanang' waliochangishwa Sh. 140,000 kila mmoja kwa ahadi ya kuanzishiwa biashara ya ufugaji kuku. Alisema udanganyifu huo ulifanyika mwaka 2016 kwa kampuni moja ya biashara kwa kushirikiana na maofisa wachache wa serikali wasio waadilifu na kujipatia Sh. milioni 42 kwa njia za udanganyifu.

"Tulikuwa tunamtafuta tangu mwaka 2016 bila mafanikio, amejisalimisha katika Ofisi za TAKUKURU tayari kwa kuanza kufanya marejesho," alisema.

Amewataka wafanyabiashara wote ambao wamewadhulumu wananchi wanyonge, kuhakikisha wanarejesha fedha na mali kwa wahusika.

**WATUMISHI NHIF**

Wakati huohuo, Jenerali Mbungo alisema TAKUKURU inawashikiliwa watumishi wanne wa Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya (NHIF) kwa mahojiano kwa tuhuma za wizi na ubadhirifu wa Sh. milioni 500.4.

"Uchunguzi dhidi ya tuhuma hizi unaendelea na hatua stahiki zitachukuliwa kwa wale wote watakaothibitika na uhalifu huu," alisema.

Aliwataka wale wote ambao wamechukua fedha za umma kwa njia za udanganyifu au dhuluma kwa wanyonge, kuzirejesha kabla rungu la TAKUKURU halijawafikia.

"Kama ambayo Rais John Magufuli ameeleza wakati akizindua Bunge la 12 jana, amesema ninanukuu "watumishi wazembe bado wapo, wala rushwa bado wapo, wezi na wabadhirifu wa mali ya umma bado wapo... utumbuaji majipu utaendelea," alinukuu.

**MILIONI 562/-**

Alisema kero nyingine iliyobainishwa ni wadaiwa sugu wa matrekta aina ya URSUS ambayo yalikopeshwa kwa baadhi ya wananchi katika mikoa mbalimbali nchini.

Alisema TAKUKURU kwa kushirikiana na Shirika la Taifa la Maendeleo (NDC) mnamo Septemba mwaka huu, ilifanya operesheni ya ukusanyaji wa madeni ya wadaiwa hao sugu katika mikoa ya Arusha na Morogoro.

"Ufuatiliaji wa madeni hayo ambao uliofanywa katika mikoa ya Morogoro na Arusha kwa muda wa siku 21, umewezesha kupatikana kwa Sh. milioni 562.1," alisema.



Kundi la watalii wa ndani zaidi ya 80 kutoka mikoa mbalimbali nchini, wakicheza ngoma ya asili ya Mkoa wa Tanga, baada ya kuwasili jijini Arusha juzi, kwaajili ya kutembelea vivutio vya utalii vilivyoko Kaskazini. **PICHA: ASRAJI MVUNGI**

# Bodi TANESCO yafuatilia utekelezaji agizo la JPM

**Na Jaliwason Jasson,** BABATI

AGIZO la Rais John Magufuli kuhusu kumalizwa haraka kwa malalamiko ya wananchi 4,000 kutounganishiwa nishati ya umeme wilayani Babati mkoani Manyara, limeipeleka Bodi ya Wakurugenzi wa Shirika la Umeme (TANESCO) mkoani huko.

Rais Magufuli alipokuwa katika Wilaya ya Babati Oktoba 25, mwaka huu, aliagiza kutekelezwa kwa mradi huo baada ya wananchi kulalamikia kuwapo kwa urasimu.

Mwenyekiti wa bodi hiyo, Dk. Alexander Kyaruzi, alisema juzi kuwa wananchi hao walioomba kuunganishiwa umeme na kukidhi vigezo, watapatiwa huduma hiyo haraka iwezekanavyo.

Kwa mujibu wa Dk. Kyaruzi, kazi hiyo itafanyika usiku na mchana ndani ya siku 30 kuanzia juzi, ili watu hao 4,000 waunganishiwe huduma hiyo. Kampuni ya Qwihaya General ya Wilaya ya Mufindi mkoani Iringa, ndiyo iliyoshinda zabuni ya kusambaza umeme katika eneo hilo.

"TANESCO mkoa, kanda na makao makuu wameweka nguvu kubwa kuhakikisha agizo la Rais linatekelezwa kwa muda mfupi na ikiwezekana wamalize kabla na kuongeza wateja zaidi ya hao wanaotakiwa kupatiwa umeme," alisema.

Akizungumza baada ya ziara hiyo, Meneja wa Tanesco Mkoa wa Manyara, Rehema Mashinji, alisema uongozi wa shirika hilo umetoa msaada mkubwa kulitafutia suluhu ya kudumu tatizo hilo.

Aliwataka wananchi hao kuwa wavumilivu wakati huu mamlaka zikiendelea kusambaza miundombinu ya umeme katika maeneo yao ili huduma iwafikie.

Meneja huyo alisema umeme huo unaosambazwa kwa sasa katika maeneo yao, unagharimiwa na TANESCO na siyo Wakala wa Usambazaji Umeme Vijijini (REA).

# Utupaji taka unavyoweka rehani ikolojia ya Mikumi

Na Sanula Athanas

UNAPOTAMKA maisha ya wanyamapori, moja kwa moja unagusa mazingira halisi wanakoishi. Vivyo hivyo, unaegemea katika asili yao ya maisha endelevu yanayojengwa kwa msingi wa mwingiliano na utegemezi.

Hapo unapata taswira gani? Mfumo mmojawapo unapoharibika, unavuruga kuwapo kwa mazingira ya asili ya upande wa pili. Hiyo ndiyo tafsiri kuu inayobeba ikolojia ya wanyamapori ndani ya hifadhi.

Moja ya kazi kuu ya wasimamizi wa hifadhi hizo ni kusimamia uhalisia wa ikolojia hiyo, jambo lililofanikiwa kwa muda mrefu lakini ndani ya miaka kadhaa iliyopita, kumeshuhudiwa madhara makubwa yanayobomoa mfumo huo endelevu.

Ni athari zinazotajwa na wadau wasimamizi kwamba zinaangukia katika sura tatu; kuzalishwa uchafu usiotakiwa hifadhini, kuharibiwa mifumo ya asili ya mazingira yakiwamo mapito ya wanyamapori na kuibuka mimea vamizi.

Makene Ngoroma, mwanzilishi wa vikundi vya kuokota taka zinazotupwa katika Hifadhi ya Taifa Mikumi (MINAPA), akirejea uzoefu wake wa miaka tisa, anashuhudia mzigo mkubwa wa taka zinazotupwa na abiria wa magari yanayopita ndani ya kilomita 50 za hifadhi hiyo.

Kwa mujibu wa Ngoroma, pia kuna athari zitokanazo na ajali za vyombo vya moto ambazo ndani yake zinajumuisha mauaji ya viumbe, pia kuzalisha taka zitokanazo na ajali, mathalan vioo vya magari vinavyovunjika.

Mwanamazingira Ngoroma (33), anawasilisha kielelezo cha ugumu wa kazi hiyo akitumia mfano wa hifadhini Mikumi kwamba kuna wakati wanaelemewa na jukumu la usafi wakiokota taka kilo 500 kwa siku.

"Hapa kwa wastani tunaokota taka kilo 300 kila siku lakini zipo siku ambazo tunaokota hadi kilo 500, hasa zile siku ambazo kunakuwa na matairi ya magari.

"Wakati mwingine magari yanapata tatizo hifadhini, hivyo wahusika wanapomaliza kurekebisha, wanaacha matairi mabovu ndani ya hifadhi. Pia kuna matairi huchomoka kwenye gari, yote hayo tunaokota. Mwongozo unatutaka tuokote kila kisichotakiwa ndani ya mita 50 kutoka barabarani.

"Vitu tunavyookota kwa wingi ni chupa za maji, makombo, nepi za watoto, makokwa ya matunda, mifuko inayotumika kubeba chakula na vyuma vinavyochomoka kwenye magari.

"Mbaya zaidi, kuna chupa za maji tunaokota zikiwa na mkojo ndani. Madereva na wasaidizi wao wanazitupa humu hifadhini baada ya kuwa wamejisaidia ndani ya magari yao, ninafikiri wanahofia wanyama wakali.

"Wanyama hasa nyani na tumbili wamekuwa wakikaa barabarani kusubiri wapewe vyakula na abiria na wamekariri hadi muda wa mabasi kupita ndani ya eneo la hifadhi.

"Wakati wa mchana lami inakuwa ya moto sana, hivyo inawaathiri nyani kwenye makalio yao maana wanalazimika kukaa barabarani kusubiri chakula cha kurushiwa.

"Pia, kuna ndege ambao wamekuwa wakitua barabarani kula zile mbegu za nafaka kama mahindi, karanga, maharage zinazodondoshwa na magari barabarani. Wote hao wanagongwa kirahisi na magari barabarani."

Mhifadhi Mkuu wa MINAPA, Kamishna Msaidizi wa Uhifadhi Mathew Mombo, ana ufafanuzi kuhusiana na hoja hiyo, akitamka:

"Kila siku kuna magari kati ya 2,500 na 3,000 yanapita hapa kwenye Hifadhi ya Taifa Mikumi na watumiaji wa magari hayo, wakiwamo abiria, wanatupa mabaki ya vyakula na kuathiri tabia za wanyamapori.

"Iko wazi kabisa kwamba kupita kwa magari haya ndani ya hifadhi, kunaleta mimea vamizi, mimea ile ambayo siyo ya asili ndani ya eneo hili," anasema.

Kamishna Mombo pia analalamika tabia ya abiria kutupa taka na kuwapa wanyama chakula hifadhini, akibainisha kuwa wengi wao wamebeba uelewa tofauti kwamba wanapofanya hivyo, wanadhani wanamsaidia mnyama kama nyani, lakini kinyume chake wanammaliza kiikolojia kwa kumwingiza kwenye maisha tofauti yasiyotakiwa kwa ustawi wake.

"Ilifika kipindi nyani na tumbili waliacha kujitafutia chakula kwenye mazingira yao ndani ya hifadhi, wakawa wanakaa barabarani kusubiri abiria wa magari wawarushie chakula," analalamika.

Mbali na utupaji wa taka za mifuko, Kamishna Mombo anasema vyakula, akivitaja mifano yake kuwa matunda kama ndizi, maembe, machungwa, hali kadhalika vyakula binafsi vilivyobakishwa na wasafiri hao, ni sehemu ya mzizi wa madhila kwa wanyamapori.

Pia, anazungumzia namna ajali na utupaji ovyo wa uchafu ndani ya hifadhi, unavyozalisha mimea vamizi na isiyotakiwa, jambo linalopanua wigo wa mazingira magumu yanayowakabili wasimamizi wa wanyamapori, ikiwamo MINAPA.

"Abiria wa magari kutupa mbegu wanapokula vyakula au matunda au vitu vyovyote vile ambavyo vinaweza vikasababisha kudondoka kwa mbegu za mimea ambayo ni vamizi katika eneo hili la hifadhi.

"Sambamba na hilo, wanapopata ajali ndani ya hifadhi, wanasababisha kunakuwa na uharibifu wa mazingira lakini pia hakuishii tu hapo, bali kusababisha kudondoshwa kwa mbegu za mimea vamizi kwenye hifadhi.

"Gari linapoanguka au kupata ajali ndani ya hifadhi, mbali na kuua wanyama wadogo watambaao ambao hawaonekani kwa urahisi katika eneo husika ambako ajali imetokea, linasababisha kudondoka kwa mbegu za mimea hiyo vamizi," analalamika.

### NJIA ZA KUKABILI

Kutokana na uhalisia kwamba suala la uzalishaji taka hifadhini ni mtambuko kwa maana ya kugusa wadau na sekta nyingi, ndani ya MINAPA nako limechukua sura hiyo.

Ili kulikabili, Kamishna Mombo anasema wameanzisha kampeni maalum ya kutoa elimu na kuchukua hatua dhidi ya wanaokiuka sheria na taratibu za hifadhi wakishirikiana na Jeshi la Polisi.

Anasema kampeni hiyo inafanyika sambamba na uongozi wa hifadhi kuanzisha vikundi vya kufanya usafi ndani ya hifadhi, hasa eneo la barabara kunakotupwa taka hizo.

"Vikundi vyetu vinafanya usafi kila siku, wanaokota taka zote na kung'oa miche ya mimea vamizi inayoota ili kulinda asili ya eneo hili la hifadhi," Kamishna Mombo anabainisha.

### MIKAKATI YA POLISI

Wilbroad Mutafungwa, Kamanda wa Polisi Mkoa wa Morogoro, anasema wameshaanzisha utaratibu wa kufanya ukaguzi wa kila mara, kufuatilia utii wa sheria na kanuni miongoni mwa madereva hifadhini.

"Tunatoa elimu kwa madereva kwa kushirikiana na watendaji wa Mikumi, tumekuwa na mpango wa pamoja wa kuwakumbusha madereva na abiria wao kuzingatia sheria na taratibu zilizowekwa kwenye hifadhi na kuchukua tahadhari.

"Tumeweka vituo maalum vya ukaguzi ndani ya hifadhi inapopita barabara ndani ya kilomita 50 ili kuwabaini madereva wanaokiuka sheria za usalama barabarani na zile za hifadhi," Kamanda Mutafungwa anasema.

### RAS NA TANAPA

Udadisi wa Nipashe kutaka kujua hatua zinazochukuliwa na serikali kumaliza kadhia hiyo, unatua mezani kwa Katibu Tawala wa Mkoa wa Morogoro, Emmanuel Kalobelo, anayeanika mkakati wa mkoa huo.


Anasema mkakati huo unahusisha kutoa elimu kwa madereva na wananchi kuhusu umuhimu wa kulinda wanyamapori walioko hifadhini Mikumi.

"Upo mkakati mwingine mkubwa zaidi ambao uko ngazi ya kitaifa ambao ni kutengeneza barabara inayopita Mikumi kwenda Kilosa mpaka Dumila ili magari yasipite tena hifadhini.

"Kikubwa, kila mmoja wetu anapaswa kuthamini manufaa ya Mbuga ya Mikumi siyo tu kwa wananchi wa Morogoro, bali pia Watanzania na dunia kwa ujumla.

"Viumbe waliopo eneo hilo ni adimu, kwa dunia ya leo wamebaki katika maeneo machache ambayo unawakuta katika maeneo yao ya asili," anasema.

Kalobelo anasema kuwa mbali na kuwa kivutio kikubwa cha watalii, Hifadhi ya Taifa Mikumi imezalisha fursa nyinyi za ajira kwa wananchi huku ikitoa fursa za uwekezaji kwenye hoteli za kitalii na uzalishaji chakula kwa ajili ya watalii wanaoitembelea.



Nipashe pia inazungumza na Kamishna Msaidizi Mwandamizi wa Uhifadhi wa TANAPA (Idara ya Mawasiliano), Paschal Shelutete, anayetaja hatua wanazozichukua ili kuilinda ikolojia ya hifadhini Mikumi.

Kamishna Shelutete anasema hatua ya kwanza inayochukuliwa ni kujenga mageti ambayo magari yatasimamishwa kisha madereva na abiria kupewa elimu kuhusu ulinzi na usalama wa hifadhi.

Kwa mujibu wa Kamishna Shelutete, hatua ya pili ni kusimika mfumo wa kamera maalum za kufuatilia mienendo ya madereva na abiria wao, akibainisha kwamba kwa sasa mchakato huo uko mbioni kukamilika.

Kamishna Shulutete anasema TANAPA pia imeongeza doria kwenye hifadhi zake zote 22 ili kutotoa nafasi kwa uhalifu huo unaotishia usalama wa hifadhi.

### KUHUSU MIKUMI

Hifadhi ya Taifa ya Mikumi ni moja kati ya hifadhi za taifa 22 ambazo zipo chini ya TANAPA.

Kwa mujibu wa Kamishna Mombo, hifadhi hiyo ilianzishwa mwaka 1964 kwa tangazo la serikali namba 465 lakini wakati ule ilikuwa na ukubwa wa kilometa za mraba 1,070.

"Miaka 11 baadaye, serikali iliona umuhimu wa eneo hilo hususani upande wa maeneo ya kusini na kaskazini kuongezwa hadi kufikia ukubwa wa kilometa za mraba 3,230 kwa tangazo la serikali namba 121.

"Kijiografia, Hifadhi ya Taifa Mikumi inapakana na wilaya tatu za Mkoa wa Morogoro ambazo ni Mvomero, Kilosa na Morogoro Vijijini. Pia imezungukwa na vijiji 19, vyote vikiwa ndani ya wilaya hizo tatu.

"Ni hifadhi ya tisa kwa ukubwa kwa hifadhi zote 22 za TANAPA. Ina wanyama wakubwa na wadogo kama vile tembo, nyati, twiga, simba, chui, nyati na swala wengi ambao ndiyo sifa tuliyonayo katika hifadhi yetu.

"Lakini pia ina aina nyingi za ndege, takriban aina 400. Watalamu wa ndege huwa wanapenda sana kuja hapa ndiyo maana inapata wageni wengi kutoka ndani na nje ya nchi," anabainisha.

RIPOTI MAALUM

## Wanahisa NICOL kuteta kuhusu kampuni yao

**Na Mwandishi Wetu**

WANAHISA wa Kampuni ya Uwekezaji ya National Investments Plc (NICOL), wanatarajia kufanya mkutano mkubwa Jumamosi ijayo kujadili masuala mbalimbali.

Kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa jana, mkutano huo unatarajiwa kufanyika kwa njia ya mtandao.

“Wanahisa watapewa ‘link’ wataingia kwenye simu zao au kompyuta zao watahudhuria mkutano huo muhimu, hivyo tunawaomba wahudhurie kwa wingi ili kuchangia kuikuza kampuni yao,” ilisema taarifa hiyo.

Taarifa hiyo ilisema baadhi ya ajenda zitakazojadiliwa ni pamoja na kupokea, kujadili na kupitisha ripoti ya wakurugenzi na taarifa za fedha kwa mwaka ulioishia 31, 2019 na tamko la gawio la nusu mwaka kwa mwaka wa fedha unaoishia 2020.

Ilitaja ajenga nyingine ni kupitisha gawio la Sh. 10 kwa kila hisa ambalo litapitishwa na wanahisa siku ya mkutano huo. Ajenda nyingine ni kupokea na kuidhinisha malipo ya wakurugenzi, kupokea na uteuzi wa wakaguzi wa hesabu kwa mwaka unaoishia Desemba 31, 2020.

“Tunahamasisha wanachama washiriki mkutano huo ambao utakuwa wa mtandao na kama watakuwa na maswali yoyote kuhusu kushiriki mkutano huo wawasiliane na uongozi wa kampuni ya NICOL,” alisema

Kampuni hiyo hivi karibuni ililipa gawio la miaka mitatu ya mwaka 2016, 2017 na 2018 ambazo zilishalipwa kupitia akaunti ya benki ya kila mwana hisa.

waka 2001 na wanahisa wachache ambao walitoa michango yao lengo likiwa ni kuwawezesha wananchi kumiliki uchumi.

Tangu kuanzishwa kwake, kampuni hiyo haikuwahi kutoa gawio hadi wananchi walipolalamika na kuchagua uongozi mpya mwaka 2012 ambapo Dk. Gideon Kaunda alichaguliwa kuwa Mwenyekiti wa Bodi.

Ilisema pamoja na changamoto mbalimbali uongozi huo mpya ulifanikiwa kuanza kutoa gawio la kwanza mwaka 2016 la Sh. 25, mwaka 2017 gawio la Sh. 26 na mwaka 2018 gawio la Sh. sita ambapo ilifanikiwa kulipa madai na malimbikizo na kodi serikali ya Sh. bilioni 1.5.

Katika kuendelea kuhakikisha inalipa gawio zuri kwa wanahisa wake, NICOL imejiwekea mikakati mipya ya kuikuza kampuni hiyo na kuwa miongoni mwa kampuni kubwa hapa nchini zinazolipa kodi na kutoa gawio zuri kwa wanahisa wake.

# Babu aanzisha darasa kufundisha Kiingereza

**Na Steven William,**
MUHEZA

WANAFUNZI wanaosoma darasa la awali mpaka darasa la saba wanaoishi katika kijiji cha Kilulu, Muheza, mkoani Tanga wanapatiwa elimu bure ya kujifunza lugha ya Kiingereza.

Hatua hiyo inatokana na Mzee Harold Ugata (70), kuanzisha darasa hilo kwa ajili ya kuwanoa wanafunzi hao. Darasa hilo sasa lina miaka mitatu tangu alipoanza kufundisha.

Kutokana na uamuzi wa mzee huyo, zaidi ya wanafunzi 10, wavulana na wasichana wanaosoma shule ya msingi ya Kilulu, wanapatiwa elimu hiyo bure kila siku jioni baada ya kutoka shuleni.

Akizungumza hivi karibuni na mwandishi wa habari hii katika darasa alilolianzisha, linalotazamana na zahanati ya kijiji hicho, Ugata alisema ameamua kufanya hivyo ili kuwawezesha wanafunzi hao kufanya vizuri katika mitihani ya somo la Kiingereza.

Ugata alisema ataendelea kujitolea kuwafundisha watoto kuanzisa chekechea hadi darasa la saba ili kipindi cha kufanya mitihani yao shuleni wapate wepesi katika kujibu maswali. Alisema hatua hiyo itasaidia kuongeza ufaulu kwa kuwa elimu katika wilaya ya Muheza imeshuka.

Mzee huyo alisema anawafundisha wanafunzi hao bure isipokuwa wazazi wenyewe huwa wanamchangia posho ya Sh. 10,000 kila mwezi kwa mtoto mmoja kwa ajil ya kununua sabuni.

Ugata alisema enzi ya utoto wake alisoma katika Shule ya Msingi ya Kilulu baadaye alifaulu na kuendelea na masomo ya darasa la tano katika Shule ya Kati ya Mkuzi kabla ya kujiunga na Shule ya Sekondari ya Tanga.

Baada ya hapo alisema aliendelea na masomo zaidi kisha kufanya kazi maeneo mbalimbali kikiwamo kiwanda cha Kamba cha Ngomeni na kiwanda cha kutengeneza baiskeli na hatimaye kisha kwenda Ulaya kusoma.

Mzee huyo alisema baada ya kustaafu kazi, aliamua kurudi nyumbani na anafanya kazi ya kujitolea kuwafundisha Kiingereza wanafunzi hao. Pia alisema yuko tayari kufundisha somo hilo katika shule kwa mkataba.

“Nawasaidia watoto wa kijiji cha Kilulu ili wapate upeo wa kusoma lakini cha kushangaza wazazi wengine wana watoto lakini hawataki kuwaleta kusoma. Kinachoshangaza wanatumia fedha nyingi kwa ajili ya michango ya harusi na ngoma.

Mzee huyo alibainisha kwamba wanafunzi wote ambao wanasoma darasa hilo, wanafanya vizuri katika somo la Kiingereza na wanawashinda hata watu wazima. Sambamba na hilo, alisema watoto hao wana nidhamu shuleni na kwa wazazi wao.

Mmiliki wa jengo ambalo Mzee Ugata ameanzisha darasa, Jumaa Amiri, alisema anamshukuru mzee huyo kwa kusaidia kuwafundisha watoto hao licha ya kwamba kiasi cha fedha anacholipwa ni kidogo kulinganisha na kazi anayofanya.

Miongoni mwa wanafunzi wa darasa hilo, Neema Jumaa na Mwasiti Ilili, ambao wanasoma darasa la sita katika Shule ya Msingi Kilulu, kwa nyakati tofauti walisema wanamshukuru mzee huyo kwa kuwafundisha Kiingereza na kwamba wanaona mabadiliko katika maendeleo yao ya elimu

Naye mkazi wa kijiji cha Kwasemwaliko, Rajabu Msumbiji, alisema kuwa mzee huyo amewasaidia sana watoto kutokana na hatua aliyochukua.

Hata hivyo, aliishauri serikali kuwaajiri wazee hao kwa mkataba katika shule kwa kuwa shule nyingi hazina walimu Kiingereza na sayansi.



Mzee Herold Mwaimu Ugata (wa pili kulia), akiwa na baadhi ya wanafunzi wake, wilayani Muheza. **PICHA: STEVEN WILLIAM**

# Uingereza yaahidi kupiga jeki sekta ya afya

**Na Cynthia Mwilolezi,**
ARUSHA

BALOZI wa Uingereza nchini Tanzania, David Concar, amesema amefurahishwa na huduma ya afya ya mama na mtoto inayotolewa katika Jiji la Arusha na kuahidi kuwa nchi yake itaendelea kushirikiana na serikali kuboresha sekta ya afya.

Akizungumza jana jijini Arusha katika ziara ya kutembelea miradi ya afya ambayo imefadhiliwa na serikali hiyo kupitia Shirika la Engender Health Tanzania, Balozi Concar, alisema amefurahi kuona huduma bora katika Kituo cha Afya Kaloleni.

“Serikali ya Uingereza itaendelea kufadhili huduma za afya Tanzania, ikiwa ni kuunga mkono jitihada za serikali ya Tanzania katika kuwapatia huduma bora za afya wananchi wake,” alisema.

Balozi Concar alisema baada ya kufanya mahojiano na kinamama wanaonufaika na mradi wanaofadhili wamebaini kuwa wataalam wa afya na wahudumu wa afya, wanafanya kazi ya kuhudumia wagonjwa kwa kufuata maadili ya kazi na kuwataka kuendelea kuwahudumia kwa ubora bila kuchoka.

“Binafsi nimefurahi kuzungumza na wagonjwa niliowakuta katika kituo hiki cha afya. Nimefurahi wakikiri wenyewe kuwa wanapatiwa huduma bora za afya kutoka kwa wataalam wa afya. Niwapongeze wataalam hawa kwa huduma bora,” alisema.

Pamoja na mambo wengine alisema wataendelea kusaidia huduma za afya kulingana na mahitaji . Naye Mkurugenzi wa Jiji la Arusha, Dk. John Pima, alishukuru kwa msaada unatolewa na serikali ya Uingereza na kwamba serikali inatambua mchango huo.

Dk. Pima alisema serikali imejenga miundombinu bora katika vituo vya afya, kikiwamo cha Kaloleni vilivyonufaika kwa kujengewa majengo ya huduma ya mama na mtoto.

Aliongeza kuwa kwa kipindi cha miaka mitano iliyopita, fedha nyingi zimeelekezwa katika huduma ya afya, hivyo kuwezesha kupatikana kwa huduma bora ikiwa ni pamoja na huduma ya mama na mtoto.

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# *Watakaoteuliwa na Rais watekeleze majukumu yao kwa maendeleo ya nchi*

**RAIS** John Magufuli, juzi alizindua Bunge la 12 la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania jijini Dodoma, ambapo aliweka dira na mipango ya serikali katika sekta mbalimbali kwa miaka mitano ijayo.

Katika hotuba yake iliyojaa matumaini kwa maendeleo ya kiuchumi, kisiasa na kijamii, Rais pamoja na mambo mengine, aliweka bayana kwamba lengo la serikali katika ngwe ya pili ya uongozi wake ni kukuza uchumi kwa asilimia nane na pia kupunguza umaskini na kuzalisha mabilionea.

Ili kutimiza yote hayo, katika masuala ya siasa, aliahidi kudumisha na kustawisha Muungano ambao umedumu kwa zaidi ya miaka 26. Alisema atahakikisha serikali zote mbili hazitawaonea haya wale watakaochezea amani na kuvunja Muungano huo ulioasisiwa na Mwalimu Julius Nyerere na Sheikh Abeid Amani Karume.

Pia katika eneo hilo aliahidi kudumisha demokrasia na utawala bora pamoja na kuendeleza uhusiano wa kikanda na kimataifa.

Kwa upande wa uchumi, alisema serikali yake itaendeleza yale yote ambayo serikali iliyaanzisha katika kipindi kilichopita kama vile maendeleo ya viwanda, kilimo, mifugo na uvuvi pamoja na kuendelea kujenga miundombinu ya barabara, reli ya kisasa viwanja vya ndege na bandari. Ili kuchochea maendeleo ya viwanda, alisema jukumu kubwa lililoko mbele yake ni kuhakikisha nishati ya uhakika inapatikana mijini na vijijini.

Huduma za jamii pia alizipa kipaumbele katika hotuba yake kwa kuweka bayana kwamba katika miaka mitano ijayo, sekta za afya, elimu na maji zitaimarishwa zaidi. Mikakati katika kuboresha huduma za afya, alisema, serikali itaendeleza kujenga hospitali, vituo vya afya na zahanati huku dawa na vifaa tiba vikipatikana bila matatizo.

Aidha katika elimu, alisema mkakati ni kujenga vyumba vya madarasa, kuongeza udahili kuanzia elimu ya awali hadi vyuo vikuu, kuongeza bajeti ya mikopo kwa wanafunzi wa elimu ya juu na kushughulikia kero zinazoikabili sekta hiyo.

Pia kwa muda mrefu kumekuwa na kilio cha ajira kwa watumishi wa umma katika sekta za afya na elimu jambo ambalo alisema serikali yake, katika miaka mitano ijayo, itaajiri watumishi wa kada mbalimbali katika sekta hizo.

Kwa ujumla, hotuba ya Rais imejaa matumaini makubwa kwa maendeleo ya nchi na wananchi wanaamini kuwa hayo yote yatatekelezwa kutokana na uthubutu aliouonyesha katika miaka mitano iliyopita.


Ni dhahiri kwamba katika kutekeleza hayo, Rais atateua viongozi na watendaji katika ngazi mbalimbali kama vile baraza la mawaziri, watendaji wa wizara, mikoa na wilaya pamoja na wakuu wa mikoa na wilaya ili kumsaidia kazi hizo kwa sekta mbalimbali na kulingana na vipaumbele vilivyowekwa.

Wateule hao wa Rais wanapaswa kutekeleza kwa dhati, juhudi na maarifa ili kuonyesha imani kwa aliyewapa nafasi hiyo, kinyume cha hapo watakuwa wanamwangusha.

Miaka mitano iliyopita ya uongozi wake, Rais Magufuli alionyesha uthubutu kwamba hana mzaha na watu wanaofanya kazi kwa mazoea, wala rushwa na wabadhirifu huku akiwaondoa wale wanaoshindwa kwenda na kasi yake, akitumia msemo maarufu wa kuwatumbua.

Kwa mantiki hiyo, wale wote watakaoteuliwa hawana budi kutekeleza wajibu wao kwa kaulimbiu ya Hapa Kazi Tu katika kuhakikisha ndoto za Watanzania kupata maendeleo zitatimia.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
**THE GUARDIAN LIMITED**
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge



Na Sabato Kasika

# *Daladala ni usafiri wa umma, kwa nini kufungulia muziki sauti ya juu?*

**USAFIRI** wa umma unaotumiwa na wakazi wa maeneo mbalimbali ya mijini, maarufu kama 'daladala', umesaidia watu kurahisisha safari zao za kwenda katika mihangaiko ya kila siku.

Wakazi wa jijini Dar es Salaam ndio watu wa mwanzo kwa kufaidika na usafiri huo tangu miaka ya 1970, kisha ukaenea kwenye miji mbalimbali nchini kwa majina mbalimbali huku Dar es Salaam mwishowe ukaitwa 'daladala'.

Pamoja na kuwapo kwa huduma hiyo ya usafiri ambao ni wa muhimu kwa wakazi wa mijini ikiwamo jiji la Dar es Salaam linalokadiriwa kuwa na zaidi ya watu milioni nne, 'daladala' zina kero zake.

Miongoni mwa kero hizo ni madereva kufungulia muziki mkubwa kana kwamba wako baa au wanaendesha magari ya binafsi, na kusababisha kero na usumbufu wa abiria wao.

Kwa wale wanaotumia usafiri huo, inawezekana walishuhudia kero hiyo au kusimuliwa jinsi ambavyo baadhi ya madereva wa daladala wanasababisha usumbufu kwenye usafiri wa umma.

Ingwa kwa baadhi ya abiria kelele hizo zinaweza kuwa ni za kawaida, ukweli ni kwamba baadhi ya madereva na makondakta wa 'daladala' si wastaarabu.

Ni vyema wakakumbushwa kuwa tabia ya kufungulia muziki hadi mwisho kana kwamba wako baa, haifai kwa kuwa huo ni usafiri wa umma si binafsi, hivyo madereva na makondakta wanatakiwa kulitambua hilo.

Lakini pia zinahitajika sheria kuweka ustaarabu katika daladala kwani kwa watu wanaoishi Dar es Salaam, kila siku na lazima wasafiri kwenye shughuli zao za kila siku na wanajazana ndani ya usafiri huo, halafu wanakumbana na kelele za muziki.

Madereva wakumbuke kuwa wanasafirisha abiria wakiwamo wengine wenye matatizo mbalimbali ambao hawahitaji kelele. Kutokana na ukweli huo, hawapaswi kufungulia muziki kama wako kwenye disko.

Wako baadhi yao ambao wakiambiwa wapunguze sauti, hutukana au kumtaka abiria aliyeomba muziki upunguzwe ashuke au apande daladala nyingine kuliko wao kupunguza sauti ya muziki.

Hata baadhi ya abiria wanaopenda sauti kubwa ya muziki, huungana nao na kutaka muziki uendelee kuwa wa sauti ya juu kana kwamba wako kwenye usafiri wa binafsi na kumbe ni wa umma.

Ingawa si madereva wote wenye mtindo huo, kwa ujumla usafiri wa umma unakutanisha wasafiri wa aina tofauti, wenye matatizo mbalimbali, hivyo ni muhimu kuheshimu abiria.

Wahusika wakilitambua hilo, hawawezi kuwakera tena abiria na wala hawatawashusha kwenye vyombo vya usafiri eti kwa sababu wanataka sauti za muziki katika daladala zipunguzwe.

Vinginevyo kama sheria haipo, basi mamlaka husika zione uwezekano wa kutunga sheria, kuliko kuacha hali ikiendelea kama ilivyo na kusababisha usumbufu usio wa lazima kwa abiria.

Kila kukicha idadi ya watu jijini Dar es Salaam inazidi kuongezeka kwa kasi hivyo umuhimu wa usafiri wa daladala nao unaongezeka, na ndiyo maana abiria ujazana katika usafiri huo.

Hivyo, suala la kuheshimu abiria kwenye usafiri huo ni la muhimu, hasa kutowasumbua kwa kelele za muziki, ambazo wengi wao huwa hawazihitaji, lakini wanalazimishwa kuzisikiliza.

Miaka ya nyuma, tatizo lilikuwa uvutaji wa sigara ndani ya daladala, lakini bahati nzuri ni kama limeisha kwa kuwa hakuna dereva anayevuta sigara abiria wakiwamo daladala.

Kwa sasa pamoja na uchafu wa baadhi ya makondakta, tatizo kubwa ni kufungulia sauti juu ya muziki na kusababisha kero na hata wakati mwingine kuumiza abiria, ambao afya zao si nzuri.Wakati mwingine wanaoshabikia sauti kubwa za muziki katika daladala ni vijana wa kike na wa kiume na hao ndio ambao wakikuta daladala haina muziki hawaipandi na wapo tayari kuchelewa shule ama nyumbani.

Hali hiyo si sawa muziki wenye sauti ya juu ndani ya usafiri wa umma haukubaliki na si ustaarabu, unakera na umaumiza wengine, hivyo madereva wanaotaka hivyo, hawana budi kuendesha magari yao binafsi.

**SAFU**

**FIKRA MBADALA**

# Kila mtu sasa ndugu wa Kamala Harris!



Nkwazi Mhango, Canada

WATAALAMU wengi wa masuala ya kisaikolojia na kijamii wanakubaliana kuwa binadamu wana hulka ya kutaka kujinasibisha na kile kilicho bora; na si vinginevyo. Jiulize ni watu wangapi wenye ndugu zao majambazi, wezi nakadhalika wanaotaka kunasibishwa nao.

Hakuna. Hivi karibuni wanaojua mahusiano ya wahindi na watu weusi walishangaa sana kuona picha mbalimbali toka India ambako waswahili huitwa kalu au nyani wakisherehekea ushindi wa binti wa kimarekeni mwenye asili ya Jamaica, Kamala Harris, alipoibuka kuwa mwanamke wa kwanza Mmarekani na Mwafrika kuwa Makamu wa rais wa taifa kubwa la Marekani baada ya rais Mteule Joe Biden kumbwaga rais Donald Trump.

Siyo India tu bali bara zima la Asia wakiwamo Wachina ambao juzi juzi waliwabagua waswahili eti wana Covid-19, wakati ilianzia huko Wuhan, China. Rejea waswahili waitwao Jarawa kwenye kisiwa cha Andaman wanavyotumika kama kivutio cha utalii ambapo wahindi huenda kuwatazama kama waswahili wafanyavyo kwa manyani ya mbuga ya Gombe kule Kigoma.

Ajabu Wachina walivyoshukiwa kuwa na Covid-19 hapa Amerika ya Kaskazini walilalamika sana wakati wakiwafanyia vibaya zaidi waswahili huko kwao.

Kwa waswahili wa Dar es Salaam na Afrika Mashariki watakuwa wameshangaa ubora wa ghafla wa Kamala. Mama huyu mwenye umri wa miaka 56 ni mtoto wa Daktari Donald Jasper Harris, Mjamaica na mama wa kihindi marehemu Daktari Shaymala Gopalan. Kwa vile urathi wa mtoto hufuata kiumeni, Harris ni mswahili mwenye asili ya Jamaica.

Pamoja na kuwa na asili ya kihindi, ni vigumu kumnasibisha na India kiasi cha kuamsha hamasa na mapenzi makubwa kwa watu wanaoishi kwenye mfumo wa kibaguzi wa caste ambapo kuoa au kuolewa na mswahili ni kitu kisichokubalika wala kuwezekana na nuksi kwa familia ya mhusika na jamii kwa ujumla.

Sina haja ya kuleta hisia za kibaguzi bali kusema ukweli japo kama jamii na watu tujifunze kuwa wakweli kwa nafsi zetu.

Kama Kamala, mswahili mwenye asili ya Jamaica angegombea hata ujumbe wa nyumba kumi nchini India, angeambulia patupu. Pamoja na ubabe wao, hapa wamarekani wanatufundisha somo la usawa ambalo limezishinda nchi nyingi hasa za Afrika na Asia.

Sijui kama kuna mswahili au mtu yeyote mwenye asili ya Afrika mwenye cheo chochote katika bara la Asia hata kiwe kidogo namna gani.

Niliwahi kusema kuwa kama rais wa zamani wa Marekani mwafrika Barack Obama mswahili wa mwenye asili ya Kenya, kama angekulia Afrika, asingekuwa rais hata wa nchi ndogo yoyote ya kiafrika kutokana na ubaguzi wa kisheria ambao hutaka mwenye kugombea wadhifa huu awe amezaliwa na wazazi wananchi wa nchi husika. Sambamba na Obama, sidhani kama Kamala angeweza kuchaguliwa kuwa rais wa Jamaica au kama nilivyodokeza hapo juu, taifa lolote la Afrika au Asia.

Hii inaonyesha namna tulivyo wabaguzi kuliko hata hawa wamerekani tunaowatuhumu ubaguzi na ukandamizi.

Hapa hapa, hebu jiulize kwa mfano, mataifa mengi ya Afrika yanakataa uraia pacha wakati mataifa tajiri ya Magharibi hayana pingamizi hili tena kwa watu maskini toka Afrika. Pingamizi hili la uraia pacha linatupa taabu waswahili tuliko huku.

Kwani hushindwa kufaidi fursa za masomo na nyingine kwa vile kuukana uraia wetu ni kikwazo nyumbani na hapa ughaibuni. Mfano, mswahili ambaye hana uraia wa Kanada ukiomba fursa kusoma chuo chochote unalipia mara tatu. Kuepuka hili, inakupasa ukae Kanada kwa miaka ili upate ukazi wa kudumu angalau uweze kupunguza makali ya huduma kama hizi ambazo ni nafuu kwa wananchi.

Ukiangalia ni kwanini taifa la Marekani limeendelea, utagundua kuwa tabia yake ya kumkubali mtu kama alivyo, hasa inapokuja kwenye mchango wake kwa taifa, ndiyo imekuwa chachu yake kubwa ya maendeleo ambayo hivi karibuni ilikuwa imedumazwa na Trump ambaye alikuwa na mtazamo wa kuangalia ndani na nyuma bila kuangalia mbele.

Kutokana na udhaifu huu, wamarekani, hasa chama cha Democrat, kiliamua kuutumia na kumuangusha.

Kwa sasa Afrika inajivuna kuwa na mwanawe kwenye jumba jeupe (White House) akiwa ameweka historia katika taifa hili ndani ya muda mfupi baada ya mwingine kukaa pale akiwa ndiye bosi. Asia nayo, kwa sasa inataka kipande cha keki cha ufanisi huu wa kinadharia ambao kivitendo, hauna lolote la kuisadia Afrika wala Asia ikizingatiwa kuwa sera za Marekani huendeshwa kitaasisi na si kwa kutegemea ni nani aliyeko ikulu japo mwenye kuwapo anaweza kuvuruga mambo kwa kiasi kikubwa kama ilivyotokea kwa Trump.

Tumalizie tuliopanzia. Umefika wakati wa Afrika kujifunza kutoka kwa wale waliotutawala linapokuja suala la uwezo wa mtu binafsi. Tuwapokee wote wenye asili yetu kama wanavyopokelewa ughaibuni ili waweze kutoa michango yao kwa bara letu pendwa.

Laiti mgombea yeyote wa urais wa Afrika au Asia angeambiwa amteue mtu kama Kamala Harris, licha ya kuchekwa na kuzuiliwa, angeonekana kama hamnazo kwa vile sheria na mazoea ya huko hayaruhusu.

Ama kweli jiwe la pembeni walilokataa waashi limekuwa bora! Ndiyo maana bara lenye kusifika kwa kubagua waswahili kama Asia sasa linajivunia binti wa kiafrika kuwa makamu wa rais wa Marekani. Tuonane wiki ijayo.

**MADONGO YA MGAGAGIGIKOKO**

# Utitiri wa vyama dhaifu hauna tija



Na Joseph Kulangwa

UONGOZI ni jukumu, ni dhima na ni wajibu katika jamii. Ili mtu uwe kiongozi, sharti uwe na sifa za kuwa hivyo, lakini pia ujiamini kuwa unaweza kubeba majukumu ya unaowaongoza, bila kuwakwaza.

Jamii nyingi za viumbe hai, huongozwa au hujiongoza, binadamu na wanyama wana taratibu za kuongozana. Wakati binadamu hupata viongozi kwa kuchaguana, wanyama hutumia misuli na mabavu kupata viongozi.

Tofauti na wanyama, binadamu hupata viongozi wao pasipo ubaguzi wa jinsi, huku wanyama huwapata kwa kuzingatia jinsi. Kwao ni madume tu ndio mara nyingi hupata kuongoza familia au koo.

Kwa kuwa wanyama hutumia maguvu na jinsi, binadamu wanatumia hekima na busara kupata viongozi, na ndiyo sababu huwa na mchakato wenye mnyukano wa hoja.

Hivi karibuni, tumeshuhudia Watanzania wakijipatia viongozi wao kwa njia ya kidemokrasia katika uchaguzi uliomalizika, ukiwa na mawazo tofauti, wapo walioupinga kuwa si wa haki na huru, lakini wapo waliouunga mkono.

Miongoni mwa waliouunga mkono na kuukubali, ni viongozi wa vyama 10 kati ya 15 vilivyoshiriki ambao walimwahidi mshindi, Dk John Magufuli wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) kuongoza kwa miaka mingine mitano na ya lala salama.

Akizungumza kwa niaba ya wenzake, aliyekuwa mgombea urais kwa tiketi ya chama cha ADC, Queen Sendiga, pamoja na mambo mengine, aliomba Serikali ifikirie vyama visivyo na wawakilishi bungeni, kupewa ruzuku ili viendeshe mambo yao.

Viongozi wa vyama hivyo visivyotaka makuu, kupitia kwa Queen, vilisema vitakuwa tayari kufanya kazi na Rais Magufuli akiona inafaa-ikumbukwe alipata kufanya hivyo katika uchaguzi mkuu wa mwaka 2015, alipomteua Anna Mghwira kuwa Mkuu wa Mkoa wa Kilimanjaro.

Mghwira aligombea pia urais kwa tiketi ya ACT-Wazalendo na kuwa mmoja wa waliompongeza Dk Magufuli kwa ushindi wake, na kuwa tayari kushirikiana naye kwa maslahi mapana ya nchi na Watanzania kwa jumla.

Naunga mkono maombi ya vyama hivyo kupitia kwa Queen, kwamba kuendesha chama cha siasa ni mzigo na bila ruzuku ni kazi nzito, na hiyo ilijidhihirisha katika kampeni, ambapo vyama vyenye musuli vilipasua milima na mabonde na mapori, kukutana na watu kuomba kura.

Vyama hivi vinyonge viliishia katika baadhi ya mikoa, huku vingine vikitembea mguu kwa mguu kusaka kura mitaani, majumbani na magengeni, na kuambulia kura chache huku vikimshuhudia Dk Magufuli akikata mbuga kwa kishindo.

Lakini pamoja na kuunga mkono, ni vema kujiuliza pia, kwani lazima Tanzania kuwa na utitiri wa vyama vya siasa, tena ambavyo huibuka nyakati za uchaguzi na kuonekana kama vyama vipya?

Hata Baba wa Taifa, Mwalimu Julius Nyerere enzi za uhai wake, alipata kupendekeza nchi iwe na vyama vichache na ikiwezekana visizidi vinne, vyenye nguvu vitakavyokabiliana na chama tawala, lakini pia vikitoa changamoto bungeni katika kuisimamia Serikali.

Ingawa Serikali hutoa ruzuku kwa vyama vyenye wabunge, cha msingi ni kwa chama husika kutumia wanachama wake, kujipatia kipato cha kujiendesha na kujiimarisha badala ya kusubiri ruzuku. Hii ikiendekezwa, ni dhahiri vyama vitageuka kuwa vikundi vya kijasiriamali na kusahau majukumu ya msingi.

Dhima ya msingi ya chama cha siasa ni kupambana kutwaa Dola, kama chama kinajiona hakina misuli ya kufanya hivyo, hakina budi kufa na kupisha chenye misuli, badala ya kuwa na vyama vya siasa vinavyounga mkono chama ambacho vinatakiwa vikitoe madarakani.

Kuomba kushirikiana na serikali ya chama kingine kwa matumaini ya kupata huruma ya ukata na kupewa ruzuku, ni kujidhoofisha na kusababisha nchi kuwa na vyama vya vipindi, ambavyo haviwezi kusaidia Watanzania. Turuhusu vyama dhaifu vife ili vipungue badala ya kuviendekeza kwa kupa ruzuku. Utitiri wao hauna manufaa kwa Taifa. Alamsiki!

## KONA YA UKWELI



Na Thobias Mwanakatwe

# Wabunge CCM mmepewa rungu sasa kazi iko kwenu

RAIS John Magufuli, juzi alihutubia na kulizindua Bunge la 12 ikiwa ni mara ya kwanza tangu amechaguliwa kushika nafasi hiyo kwa awamu ya pili ya miaka mitano.

Katika hotuba yake, Rais Magufuli alipata nafasi ya kutoa dira na mwelekeo wa serikali yake kwa miaka mitano ijayo.

Rais Magufuli ambaye pia ni Mwenyekiti wa Chama Cha Mapinduzi (CCM), katika hotuba yake hiyo pia alitaka wabunge wa CCM kutetea maeneo yao kwa kutoa changamoto zilizopo kwa nguvu zao zote na ikiwezekana hata kwa kufokea mawaziri.

Kauli hiyo ya Rais Magufuli inawapa nguvu wabunge hao ambao tangu uchaguzi mkuu uishe na chama tawala kuibuka na ushindi wa kishindo kwenye ngazi zote za urais, ubunge na udiwani, pameibuka mjadala mkubwa sana mitaani kwa watu kuhoji na kutabiri bunge jipya litakavyokuwa hasa ikizingatiwa bunge hilo kutawaliwa na chama kimoja tu kwa zaidi ya asilimia 95.

Wengi wanajiuliza bunge hili litakavyokuwa na namna mijadala itakavyokuwa na kutawaliwa, wengi wakisema huenda likawa bunge lisilo na makucha litakalotawala tu kusifiana, pongezi na bunge bubu ambalo halitakuwa na nguvu kuisimamia, kuihoji na kuiwajibisha serikali.

Wengine wamefika mbali kwa kutabiri huenda bunge hili lisiwe na msisimko na joto kubwa tena la mijadala mizito hasa ikizingatiwa idadi kubwa ya wabunge wake kuwa wa CCM tu ambao wengi wao wanasema wamezoeleka kuwa ni wabunge wa ndiyo mzee, watu wa kugonga meza tu na wajumbe ndiyo.

Maoni ni mengi kulihusu bunge hili lililoanza wiki hii kwa kuvunja rekodi ya kuwa bunge lenye idadi kubwa ya wabunge wa chama kimoja tawala toka tuingie mfumo wa vyama vingi mwaka 1995.

Sasa kwa hali kama hii na hali ilivyo wabunge wa CCM wana kazi kubwa sana ya kuondoa mitazamo hii hasi ambayo imejengeka huku mitaani ili kutoa imani yake kwa watu. Kwa bahati nzuri sana

Kwa mitazamo hii ya watu na kauli hii ya mwenyekiti, ni dhahiri unakuja wakati maalum ili kuondoa dhana ya kwamba ukiwa Mbunge wa CCM huwezi kuikosoa na kuihoji serikali kwa nguvu zako zote.

Mitazamo hii yote inaawaambia wabunge wa CCM kwamba wanayo kazi ya ziada kuuaminisha umma na kuthibitisha tofauti kwamba hawawezi kuihoji serikali.

Bunge hili kwangu kwa wabunge wa CCM ni kwenda kuondoa mitazamo hii kwa kuisimamia vilivyo Serikali. Imani hii kubwa ambayo Watanzania wameipa CCM inapaswa kulipwa kwa kuchapa kazi kubwa sana isiyo na mashaka ndani yake.

Kwa wabunge hili lisiwe bunge bubu au la ndiyo serikali kwa sababu ya kuwepo chama kimoja tu. Wabunge wanayo kazi ya kuwaaminisha Watanzania na kuwathibitishia kwa kuhakikisha wanaihoji kweli serikali na kuhoji kila aina ya maamuzi ya serikali na kutotoa nafasi kwa hoja zinazoonekana hazina manufaa kwa nchi kupita.

Kwangu, wabunge wa CCM wanayo kazi ya ziada kuthibitisha kwa umma waliotoa mamlaka hiyo. Wananchi wanataka kuona hoja na kero zao zinasemewa vilivyo bungeni, serikali ikibanwa kweli kutoa majibu ya kero za wananchi na namna zitakavyotatuliwa.

Kwa hiyo kwa wingi wao wanapaswa kutanguliza maslahi ya wananchi wao kwa kuondoa haya makandokando ya hapa na pale kwamba bunge hili kwa sababu limetawaliwa na chama kimoja tu basi litakuwa la ndiyo tu mzee.

Sasa kwa mazingira haya, wabunge wa CCM wanahitaji sana kuonyesha tofauti na walivyokuwa wakidhani watu kuwa watakuwa watu wa 'ndiyo mzee'. Kila la heri wabunge wa CCM.

**MUNGU IBARIKI TANZANIA, MUNGU RIBARIKI BUNGE LA 12**

## DARASA LA NDOA



Na Mch.Dk. Enock Mlyuka 0744000066

# Kanuni ya kuacha, kuambatana na kuwa mwili mmoja

WATU wengi wanatamani kuoa au kuolewa. Ni jambo jema kwani Mungu alianzisha taasisi ya ndoa ili watu waitamani, waingie na kuifurahia.

Hata hivyo, watu wengi wameivamia taasisi hii pasipo kujua uneyeti, maana na misingi yake. Wako wanaofikiri kuwa ndoa ni jambo la kawaida tu. Wanatumaini kuwa baada ya kuoa au kuolewa, furaha na starehe zinakuja zenyewe bila kutengenezewa mazingira.

Vijana wengi hawaandaliwi vya kutosha kabla ya ndoa, hivyo wengi wao wanaingia wakiwa na ufahamu mdogo kuhusu taasisi hii.

Kwa bahati mbaya sana, jitahada kubwa zimewekwa katika kuandaa sherehe kubwa za arusi na siyo kuwandaa vijana kuwa waume na wake bora. Lengo la mada hii ni kuelimisha wanandoa na wanandoa watarajiwa, kuhusu maana ya kuwaacha wazazi, kuambatana na mke na kuwa mwili mmoja katika ndoa.

Maneno kuacha wazazi (baba na mama), kuambatana na mke na kuwa mwili mmoja ni maneno ambayo yamezoeleka sana miongoni mwa watu wengi. Aidha, yamekuwa yakitumika katika ndoa nyingi na katika kadi za mialiko. Mara nyingi watumiaji wa maneno hayo wamekuwa wakiyatumia kwa mazoea bila kutafakari uzito na maana yake.

Ndoa ni taasisi ya kijamii iliyo huru na inayojitegemea. Hivyo, Kuwaacha wazazi kuna maana zaidi ya kuondoka na kwenda kuishi mahali pengine na mke au mume. Kuwaacha wazazi kunamaanisha kuwa tangu siku ya harusi uhusiano wa mwanamume na wazazi wake unapunguzwa na uhusiano mkubwa utakuwa na mke wake.

Neno kuacha linaonyesha sababu, umuhimu na maana ya mwanamke kwa mwanamume, kutokana na mpango wa Mungu wa uumbaji. Neno kuacha (leave) linabadili uhusiano wa kibinadamu uliozoeleka kati ya mume na wazazi wake.

Hii ndiyo kusema kwamba mwanamume anapooa uhusiano wake na mkewe ni jambo la msingi na kipaumbele cha kwanza. Kwa msingi huu, vijana wanapoandaliwa kuingia katika maisha ya ndoa, wanahitaji kuandaliwa kisaikolojia kukabili mabadiliko haya, yaani kuacha wazazi na kuambatana na mwenzi na si wazazi. Vijana waandaliwe kuondoka, kujitegemea na kuwa na uhuru wa kuendesha maisha yao ya ndoa. Aidha, Wazazi wao nao wanahitaji kufahamu badiliko hili muhimu, kwani mambo hayatakuwa kama yalivyozoeleka hapo awali.

Katika kuacha, kunajengwa familia mpya ambapo wanandoa wanahitaji kujenga utambulisho wao, hivyo kujitenga kwa kiasi fulani, kutoka kwa wazazi kimwili, kihisia, kiufahamu, kiuamuzi na kimapato. Kwa maana nyingine, vijana wanapaswa kuwa na uhuru na faragha binafsi; uhuru katika kufikiri mambo yenye faida kwao wawili na ndoa yao; uhuru katika kufanya maamuzi mbalimbali yanayohusu maisha yao na wazazi wao au ndugu zao; uhuru katika mapato yao na matumizi yake kwa ustawi wa familia yao.

Wanandoa wanakuwa na mamlaka na utawala kamili. Kwa hiyo, Wanandoa kuendelea kuwa tegemezi kwa wazazi wao, kuishi kwa mashinikizo na kuongozwa na watu wengine ni dalili ya kutokukua. Hali hii huondoa uhuru na kujiamini kwa wanandoa katika kuendesha na kusimamia maisha yao ya ndoa.

Mtu akiwa ameoa au kuolewa maana yake ni kwamba, amekuwa mtu mzima mwenye uamuzi. Kwa mantiki hiyo, mwanandoa kusubiri kuambiwa afanye nini au kufuata kila kitu wazazi au ndugu wanachotaka au wasichotaka, ni kuikosea ndoa na matokeo yake ni misuguano na ugomvi ndani ya ndoa kwani nafasi ya mwenzi inakuwa haipo tena.

Ikumbukwe kuwa, wazazi wetu au ndugu zetu hawana tofauti na watu wengine wowote kwenye jamii au duniani. Hata sisi huenda tu wazazi pia. Hii inaonesha kwamba, kuwa mzazi haina maana ya mtu kuwa na thamani zaidi ya mwingine. Sifa ya awali ya kila binadamu ni ubinadamu wake, hizo sifa nyingine za u-baba, u-mama, u-dada au u-kaka ni utambulisho wa kijamii.

Baba au mama, kaka au dada wanastahili kuheshimiwa nasi kama binadamu kwanza, halafu kama ndugu au wazazi. Lakini, kuwa ndugu au wazazi hakuwapi watu hawa haki wala uwezo wa kuingilia ndoa za watoto wao au ndugu zao.

Pamoja kwamba mtoto hakui kwa mzazi, lakini inapofikia hatua ya ndoa, kuna mipaka ya kutunzwa na kuheshimiwa na wazazi ili ndoa ikue. Kukua ni pamoja na kujua kwamba, hata mzazi anaweza kukosea kama binadamu mwingine yoyote.

Mzazi anapoanza kutoa amri au kuingilia ndoa yako, usimtazame kama mzazi tu, bali kama binadamu. Ukimtazama kama binadamu utaona udhaifu wake na utakuwa tayari kuukabili.

Kama mzazi atatumia utambulisho wake wa u-baba au u-mama kutaka ufanye ayatakayo wakati unajua siyo ya haki wala kujenga, bali yanatokana na udhaifu wake wa kibinadamu, ni muhimu kupingwa kwa hekima na kwa nguvu zote kwa maslahi ya ndoa yako.

Ni vyema ifahamike kuwa kuacha wazazi haimaanishi kutelekeza au kuondoa nafasi ya wazazi kwa watoto wao, bali kutoa uhuru kwa watoto wao waliooana kuendesha maisha yao ya ndoa bila kuingiliwa wala kupokea amri kutoka kwa wazazi.

Kufanya hivyo ni sehemu ya kuheshimu mipaka na ndoa ya watoto wao na kutambua kuwa, sasa ni watu wazima wenye uwezo wa kufanya uamuzi na wenye majukumu mapya.

**Itaendelea Jumapili ijayo**

**■DK. Mlyuka ni Mchungaji wa Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania na Mkurugenzi Mtendaji wa Asasi ya Tanzania Marriage and Child Care Foundation (TaMCare) inayojishughulisha na masuala ya Ndoa na Malezi ya Watoto. Kwa maoni na ushauri wasiliana naye kwa baruapepe: info@tamcare.or.tz**

# MAISHA

NOVEMBA 15, 2020
Nipashe
Baba, Mama na Mwana
Jumapili




## HARUSI

Ukurasa 12



Ukurasa 15

## MAISHA NI NYUMBA

Fahamu aina ya uzio kwenye nyumba yako



## KABABU ZA NYAMA

Ukurasa 14



## MACHO YA MAHABA

# Je unajua kungumanga inakupa jibu?

Ukurasa 14

# Mwisho wa urafiki na mwanao huanzia hapa...

**Na Moses Ismail**

ANAPOKUWA mchanga, baba huonyesha mapenzi makubwa kwake na anatenga hata muda wa kurudi nyumbani mapema ili kucheza naye. Haijalishi awe mtoto wa kike au wa kiume

Hili linaendelea hata anapotimiza miaka minne na pengine hata mitano, na wakati mwingi baba akiwa kwenye 'baraza' na marafiki zake, huwapa 'stori' za mtoto wake kuhusu mambo fulani ya kitoto anayofanya.

"Mwanangu bwana, jana kanifurahisha sana." Atapigastori na wenzake akiwaeleza kituko fulani alichofanya mtoto wake na wenzake nao watacheka.

Na baba huyu huyu anapokaa sebuleni, pengine kusoma gazeti au kaangalia TV, haoni kero kabisa pale mtoto huyu anapomdandia mapajani na kuanza kumuongelesha au kumuuliza maswali fulani ya kitoto, atamjibu kitoto pia.

Tatizo linaanza pale mtoto anapoongezeka umri, unapofikia miaka sita na kuendelea, ule urafiki baina ya mtoto na baba unaanza kupungua kabisa. Baba anapoteza kabisa ile hamu ya kukaa na mtoto wake.

Maswali na michezo au kitendo cha mtoto kukaa pembeni mwa 'ubavu' wa baba wakati baba akiwa sebuleni, inaanza kuwa kero kwa baba, atamwambia: "Hebu kaa pale, tunagusanagusana nini? Huwezi kukaa pake yako?"

Haiishi hapo, ile tabia ya kumwambia kwa upole; "angalia shati lako lilivyochafuka, haya nenda kavue," sasa inabadilika, baba anapoteza upole wake na kuanza kusema: "Uona unavyojichafua, hebu toka hapa."

Hili linaongezeka kwenye jambo moja, la pili na baadaye linakuwa la kawaida kwa kila jambo analokosea mtoto, hakanywi tena kwa upendo, anakuwa wa kufokewa na kwa sababu hiyo anaanza kujiweka mbali na baba.

Hapa ndipo unapoanza kushangaa na kujiuliza, hivi ulifia wapi ule upendo baina ya baba na mtoto ulioanza tangu siku ile mtoto alipozaliwa na ukaendelea kuwapo mpaka mtoto alipokuwa na miaka mtano au hadi sita? Nini kimemkumba baba huyu?

Kiasili wazazi wote, hasa baba, wanapenda kuona mtoto wao wanaoanza 'kujitegemea' kwa mambo madogo kama kuomba maji au kuvua nguo wakati wa kujisaidia, wanaamini watoto hao wanaakili za kufanya mambo mengine.

Wanapoona mtoto anafanya makosa, ya kitoto, akiwa na umri huo wa kujitegemea, wanahisi wanafanya mambo hayo kwa makusudi na hapo ndipo urafiki wa utotoni baina ya mtoto na baba, pengine hata mama, unapokufa."

Katika hali kama hiyo, inawezekana kweli mzazi akaendelea kupatana na mtoto wake na kumpenda tena kama alivyokuwa mtoto mchanga au alipokuwa chini ya miaka minne?

Inawezekana iwapo wazazi watafahamu kuwa mtoto anapokuwa katika umri wa miaka 0 hadi miaka 14, akili bado inakuwa haijakomaa vizuri kuweza kuzingatia mambo kama watu wazima, ni kipindi ambacho watoto hufanya makosa mengi na wanahitaji kuvumiliwa.

## NA HAMIS KIDAGO

0657 207168

# QUIZ

### LE QUIZ DU WEEK

1. Nyumbua kitenzi "Être" kama maelekezo yanavyoonesha hapo chini.

Conditionnel

Présent

Je ................

Tu ................

Il/elle ................

Nous ................

Vous ................

Ils/ells ................

Passé

J' ..........................

Tu ..........................

Il/elle ..........................

Nous ..........................

Vous ..........................

Ils/elles ..........................

2. Nyumbua kitenzi "Être" katika "Infinitif" présent na passé.

- Présent =
- Passé = ...............

3. Weka kitenzi "Être" katika Participe présent na passé.

- Présent = ...............
- Passé = ...............
  ...............

4. Pangilia kitenzi "Être" katika Impératif présent na passé.

- Présent = ............
  ............
  ............
- Passé = ...............
  ...............
  ...............

### MAJIBU YA WIKI ILIYOPITA

Le quiz du week – end

- Nyumbua kitenzi "Être" kama maelekezo yanavyoonesha hapo chini.

Conditionnel

Présent

Je serais

Tu serais

Il/elle serait

Nous serions

Vous seriez

Ils/ells seraient

Passé

J' aurais été

Tu aurais été

Il/elle aurait été

Nous aurions été


Vous auriez été

Ils/elles auraient été


- Nyumbua kitenzi "Être" katika "Infinitif" présent na passé.
  - Présent = être
  - Passé = avoir été
- Weka kitenzi "Être" katika Participe présent na passé.
  - Présent = étant
  - Passé = été
    ayant été
- Pangilia kitenzi "Être" katika Impératif présent na passé.
  - Présent = sois
    soyons
    soyez
  - Passé = aie été
    ayons été
    ayez été

## WATOTO

# PAKA RANGI



## CHEKA KIDOGO



Ng'ombe mdogo huitwa Ndama, je, Ng'ombe dume huitwa nani?

**Angalia jinsi wanawake walivyokuwa na huruma, hata kama mwanamume akifanya kosa anajikuta akihangaika kwa kumuonea huruma.**

**MUME:** Fungua mlango!

MKE: Leo sifungui! Nimechoshwa na ulevi wako.

**MUME:** Kama hufungui najitupa kwenye hili shimo nife kabisa.

**MKE.** Kufa huna faida yoyote duniani!

**MUME** kachukua jiwe kubwa kalitupa kwenye shimo chubwiiiiiii!

**MKE:** Baba John jamani, weee Baba John ebu usifanye utani...kafungua mlango haraka na ghafla mume kaingia ndani.

**MKE:** Usirudie tena utani wa namna hii, unanipa presha.

# MAISHA NDIVYO YALIVYO
Na Flora Wingia



## Mke wangu kaolewa na wanaume watatu, sasa eti anataka turudiane kwa masharti

KARIBU tena msomaji wangu tupate chachandu za Maisha Ndivyo Yalivyo. Yapo mambo ukiyasikia unabaki kujiuliza maswali mengi. Lakini kwa ufahamu wangu, hakuna jambo linalotokea kwa bahati mbaya pasipo kuwapo chanzo.
Unapoona kinatokea kitu, kilianzia mahali fulani kwani kila tatizo lina chanzo. Watu wengi leo wana shida mbalimbali katika maisha yao, lakini hawajui zilianzia wapi. Wanachukulia kila jambo ni kawaida kumbe lipo chimbuko lake.
Hata daktari anapoonana na mgonjwa, kitu cha kwanza hufanya mahojiano kwa kumuuliza maswali kadhaa ikiwamo, anajisikiaje, tatizo ni nini, lilianzaje, lilianza lini na kadhalika. Baada ya hapo atamfanyia uchunguzi kupitia vipimo kujua chanzo hasa cha tatizo lake, ndipo ampatie tiba. Hiyo ni kanuni ya kitabibu.
Matatizo mengi ya wanadamu huanzia kwenye ulimwengu wa roho (ule ulimwengu usioonekana kwa macho).
Mtu anaweza kuumwa na kufanyiwa vipimo vyote lakini ugonjwa hauonekani.
Akiombewa na mtumishi mwenye nguvu ya Mungu anapona. Kumbe chanzo ni pepo au nguvu za giza ambazo hazionekani kwa macho ya kibinadamu.
Wengine matatizo waliyonayo yanatokana na roho za mizimu au maagano ya ukoo wao ambayo yaliwekwa na mababu na sasa hawapo, yanashambulia familia zao.
Na kibaya zaidi, nguvu hizi hutesa maisha yanapofikia hatua fulani ya mafanikio.
Msomaji wetu mmoja aliyejitambulisha kwa jina la G. Msacky wa Kilimanjaro alisoma moja ya makala za safu hii wiki za karibuni akanitumia ujumbe ufuatao;-
"Kweli hata mimi yamenikuta, nilioa mwanamke ambaye kwao hawakai kwa mume. Huyu wangu ukiacha mimi kumuoa, alishaolewa mara mbili, na kote huko kila mwanamume alizaa naye watoto wawili. Mimi nina watoto wanne naye.
Sasa cha ajabu, kanikimbia akaenda zake kupanga nyumba. Halafu akanifuata eti tuendelee kimahusiano lakini kwa masharti kwamba yeye aendelee kukaa kwake na mimi nikae kwangu. Anti, je, hiyo inawezekana kweli? Hebu nipe ushauri nifanyeje niko njiapanda".
Mpenzi msomaji, bila shaka umemuelewa mpendwa huyu changamoto anayokabiliana nayo. Hapa shida kubwa ipo kwa mwanamke huyo. Anateswa na roho ya mitala ambayo humfanya mtu kuolewa na kuachika au kuoa na kuachwa. Roho hii inasumbua watu wengi wakiwamo wanaotokana na familia za kichifu au kitemi zenye ndoa za wake wengi.
Tanzama mwanamke huyu ameishi na wanaume watatu na kuzaa nao watoto ambao sasa wanafikia wanane. Bado anataka kurudia mahusiano na mume wa kwanza aliyeleta kilio chake hapa. Mama huyu hajajua chanzo cha kuhangaika kwake huku kunatokana na nini.
Hilo ni tatizo kubwa alilo nalo. Lakini akitulia na kuangalia asili yake vizazi vya nyuma anaweza kugundua kwanini anaishi maisha ya aina hiyo.
Pengine tatizo lilikuwepo kwa bibi yake au kwenye ukoo wake. Hiyo ni roho ya mitala kama nilivyodokeza awali.
Tatizo kama hili la kuolewa na kuachika au kuoa na kuachwa, ni muhimu mtu arudi nyuma kutafuta chanzo, je, babu na bibi walidumu kwenye ndoa? Utavumilia sana lakini utaishi kwa kuteseka. Lengo la hizi roho ni ili uende kwingine usitulie mahali pamoja.
Komboa kizazi chako kwa kuchunguza chanzo mapema. Matatizo mengine yanatokana na dhambi zilizotendwa na wazazi, mababu na mabibi kupitia koo zetu. Walifanya matambiko, walitoa kafara ikiwa ni pamoja na kuua. Hicho chaweza pia kuwa chanzo kinachowaletea watu wengi matatizo katika hatua mbalimbali za maisha yao.
Kwa mfano, Mungu anafunua katika moja ya maandiko yake kwamba " Babu zetu walitenda dhambi, na hata sasa hawapo, na sisi tumeyachukua maovu yao." Tunachukua adhabu zao kwani hawakupata nafasi ya kutubu.
Yaani tunakula mti wa dhambi. Yote hayo husukumwa na chanzo. Ili ujue chanzo lazima uchunguze mzizi wake kwani maovu ni matunda ya dhambi.
Unachofanya leo kinaweza kugharimu kizazi chako.
Niishie hapa msomaji wangu, ili nawe upate nafasi ya kuchangia kwa maoni au ushauri kwa ndugu yetu Msacky.
Ukiwa tayari, tuma ujumbe mfupi kupitia 0715268581. Namba hii ipo pia WhatsAPP.
Tukutane wiki ijayo.

# NAWAZA KWA SAUTI
Na Salome Kitomari



## Lazima kutibu mzizi wa tatizo suala la saruji

BEI ya saruji katika maeneo mbalimbali nchini imependa huku ikikosekana kabisa katika baadhi ya wauzaji wa jumla na rejareja, kiasi cha baadhi ya wananchi kusitisha shughuli za ujenzi.
Kwa mikoa yenye viwanda vya saruji kumekuwa na ongezeko la bei ya rejareja kwa maeneo yote ya mjini na vijijini ikiwa ni kati ya Sh. 3,000 na 8,000.
Katika baadhi ya maeneo viongozi wamefanya ziara kwenye viwanda vya saruji na kutoa maelekezo ya kutopandisha bei ya bidhaa hiyo, huku kukiwa na maelekezo ya kuchukua hatua kwa wote wanaopandisha bei.
Wengi hutegemea bidhaa hiyo kwa ajili ya shughuli za ujenzi wa nyumba na miundombinu mingine, baadhi wanaeleza kushindwa kuendelea na kuiomba serikali kuingilia kati kuhakikisha kinachosababisha bei kupaa kinashughulikiwa.
Katika hotuba ya bajeti ya Wizara ya Viwanda na Biashara kwa mwaka 2020/21, ilieleza kuwa nchi imejitosheleza katika baadhi ya bidhaa muhimu zinazozalishwa nchini zikiwamo saruji, marumaru, nondo, mabati na vifaa vya umeme.
Hali hiyo ilitokana na wizara kuhamasisha wawekezaji kujenga viwanda vipya pamoja na upanuzi wa viwanda vya zamani vya saruji kama Tanga na Mbeya na kuanza kwa uzalishaji wa viwanda vipya kikiwamo kiwanda cha Kilimanjaro cha mjini Tanga kilichoanza kazi mwaka 2017.
Hotuba hiyo ilibainisha kua uzalishaji uliongezeka kutoka tani milioni 9.1 kwa mwaka 2019 ikilinganishwa na tani milioni 4.7 mwaka 2015.
Aidha, uzalishaji halisi ni tani milioni 7.4 huku mahitaji halisi yakiwa ni zaidi ya tani milioni 4.8, na kwamba kuna ziada ya tani milioni 2.6 ambazo huuzwa nje ya nchi zikiwamo za Rwanda, Burundi, Malawi, Zambia, Jamhuri ya Kidemokrasi ya Congo na Msumbiji.
Tayari serikali imesema wanaoongeza bei ni walanguzi kwa kuwa viwada havijapandisha bei, huku wakitaja bei inayopaswa kuwa ni Sh. 14,500 kwa mfuko wa kilo 50.
Nimeona wakuu wa mikoa na wilaya kadhaa wamefanya ziara kwenye viwanda na kutoa maelekezo ya kuongeza kasi ya uzalishaji huku wakiwaonya wanaopandisha bei ya bidhaa hiyo kuwa ni makosa wanapaswa kufuata utaratibu wa bei elekezi.
Kutokana na hali halisi iliyopo kwenye maduka ya rejareja, bado nawaza kwa sauti kwa mzizi wa tatizo haujashughulikiwa kwa kuwa bado inahitajika kujua kwa nini saruji imeadimika, nini kimesababisha iadimike na nini kinafanyika kuhakikisha inapatikana.
Maeneo mengi hakuna saruji, wauzaji wa rejareja wanasema walipeleka magari kiwandani kwa ajili ya kupata bidhaa hiyo bila mafanikio kwa kile walichoeleza kuwa kuna foleni ndefu.
Ni lazima hatua madhubuti kukabiliana na hali hii zichukuliwe vinginevyo bado tatizo litakuwepo kwa kuwa kama ilifichwa ili ionekane bei imependa maana yake itazidi kukosekana mtaani.
Mathalani, katika moja ya maduka niliotembelea hivi karibuni jijini Dar es Salaam, muuzaji alisema ana mwezi mmoja hajauza bidhaa hiyo na hajui lini ataipata. Maana yake ni kuwa bado kuna tatizo na haipatikani.
Kama saruji itapanda bei maana yake gharama za ujenzi zitaongezeka kwamba muuza tofali naye atalazimika kupandisha bei kwa kuwa bidhaa haipatikani.
Kwa kuwa serikali ilishaeleza kuwa kuna uzalishaji wa ziada wa bidhaa hiyo, maana yake inatosheleza soko la ndani na sasa tuna ziada ya kuuza nje ya nchi.
Inapokuwa tofauti ni lazima kutosheleza mahitaji ya soko la ndani kwanza, ili kutotengeneza uhaba ambao utapandisha bei ya bidhaa hiyo na kusababisha maumivu kwa mwananchi mmoja mmoja au taasisi inazotegemea saruji kwa shughuli mbalimbali za maendeleo.
Ni muhimu sana wahusika kwenda hadi kwenye mzizi wa tatizo kuhakikisha linamalizika, kwa kuwa haitafaa sana kuagiza wauzaji wadogowadogo huku bidhaa hiyo haipo kwao, na wakiipata wanainunua kwa bei ya juu na ili wapate faida ni lazima kupandisha bei kidogo.
Kama wapo wanaofanya hujuma wajulikane na kuchukuliwa hatua ili iwe fundisho kwa wengine wanaofanya au wanatarajia kufanya hivyo.
**Mungu ibariki Tanzania**









Bwana na Bibi Christopher Mwakangale, wakifurahia baada ya kufunga ndoa katika Kanisa la Kiinjili la Kilutheri (KKKT), Usharika wa Songea, mji wa Tunduma, Novemba 7, mwaka huu.

# MITINDO

# MWANAMUME PIGA, UA LAZIMA AWE NA NGUO HIZI....



WANAMUME ni kiumbe wa ajabu, huwa hajali sana kuvaa au suala zima la kujipenda.Anaamini suala hilo linawahusu sana wanawake, jambo ambalo si kweli.
Kulingana na wataalam wa mavazi, hata kama mwanamume hana tabia ya kupenda kuvaa mavazi ya gharama, lakini ni muhimu kuwa na nguo ambazo zinampendezesha na kumtoa tofauti.
Lazima ieleweke kwamba badala ya kufuata mitindo, nguo zifuatazo ni muhimu kuwa nazo.

1. Fulana za pamba
Kama unahitaji nguo inayoweza kudumu kwa muda mrefu, basi fulana iliyetengenezwa kwa pamba kwa asilimia mia. Tafuta fulana za rangi tofauti ili kukupa muonekano tofauti kila siku.

2. Fulana za Polo
Mwanamume yoyote anatakiwa kuwa na fulana za Polo, kwani nguo hizi zinafaa sana kuvaliwa sehemu yoyote kwa wiki mzima.

3. Mashati ya kawaida
Nunua mashati ya kawaida, iwe ya mikono mirefu au mifupi, ni kuvaa nguo hizi na suaruali za Jeans. Inapendeza ukiwa na mashati ya rangi tofauti ndani mwako.

4. Bukta
Kwa kuzingatia hali ya joto inayotawala sehemu kubwa ya Tanzania, bukta ni nguo muhimu kukabiliana na hali hiyo. Kuna aina nyingi za bukta na zenye rangi tofauti, nunua zile unazoweza kuvaa usiku, matembezi ya wiki au ukiwa nyumbani kwako nyakati za jioni.

5. Suruali za kawaida
Suruali za aina hii zina faraja na zinavaliwa kwenye mazingira mbalimbali. Pia, unashauriwa kuwa na za rangi tofauti. Nguo hizi huvaliwa na mashati, fulana na viatu vya aina mbalimabli.

6. Jeans
Jeans zinaweza kuvaliwa mahali popote na siku yoyote ndani ya wiki.
Ni muhimu kuwa nazo za rangi na mitindo tofauti kutokana na vazi hili kukubali kuvaa na aina yoyote ya nguo na viatu.
Jambo muhimu kujua saizi yako ile upendeze zaidi, pia jeans zenye ubora huwa na gharama ya juu, usiogope kwani nguo hizi zinadumu kwa muda mrefu na huwa hazichuji mitindo yake.

## UREMBO

# MACHO YA MAHABA

# Je, unajua kungumanga inakupa jibu?



TUNDA la mti wa mkungumanga, limekuwa na hadithi nyingi za kuvutia, lakini maarufu ni zile zinazoelezea jinsi zinavyomfanya mwanamke kuwa na haiba nzuri na mvuto wa kipekee wa kimahaba pale anapokula tunda lake.

Mbegu ya tunda la kungumanga, limekuwa maarufu katika maeneo ya Pwani, mara nyingi wanawake hutumia kwa ajili kuongeza mvuto hasa kwenye macho.

Unapokwenda mikoa ya Tanga, Pwani na Zanzibar, ni jambo la kawaida kukutana na wanawake wanaotumia kungumanga kwa ajili ya kuonesha urembo wao kwenye macho.

Kitaalamu bado haijathibitika athari ya kiafya inatokana na mbegu hizo, lakini mtu anapokula macho yake yanapata ulegevu na kubaki yanashindwa kuangalia vyema, hivyo macho yanaonekana kama yameelemewa wakati mtu hajakunywa pombe ya aina yoyote.

Mwanamke aliyekula kungumanga anakuwa na mvuto wa kipekee, mara nyingi watu uhusisha matumizi ya mbegu hizi kivutio katika mahaba kwa wapenzi.

MATUMIZI YAKE

Kungumanga hutumika baada ya kusagwa mbegu yake, na kasha huchanganywa katika glasi ya juisi, chai au uji kabla ya mtu kunywa

Baada ya dakika tano, mtu hupata matokeo kwa macho huwa katika hali ya ulegevu imara na wenye mvuto wa kipekee.

Kimsingi kungumanga ni sawa na kileo, hivyo hupaswi kutumia mara kwa mara bali pale unapotaka kukutana na mwenzi wako ili kukupa msisimko halisi.

Wachambuzi wa urembo, wanasema mbegu hizo ni muhimu katika urembo kwa Mwanamke pekee.

## MAPISHI

### Na Mary Geofrey

# KABABU ZA NYAMA



**Mahitaji**

MINOFU ya nyama ya ng'ombe, kuku au samaki, yai moja, kipande kimoja cha mkate, pilipili hoho moja, kitunguu maji kimoja, kitunguu saumu kimoja, karafuu iliyosagwa, chumvi na limao.

Namna ya kuandaa

Kitunguu maji na pilipili hoho, vyote vikatwe vipande vidogo, ponda kitunguu saumu kwenye kinu, halafu viweke pembeni.

Andaa nyama ya samaki, kuku au ya ng'ombe kwa kukata vipande, ioshe, kisha ichemshe na weka ndimu na chumvi.

Nyunyuzia pilipili manga, usiongeze maji kwenye nyama, acha ikauke halafu weka kitunguu.

Loweka kipande cha mkate kwenye maji, kitoe na kikamue kisha changanya na mayai yaliyopasuliwa na kukorogwa na kuchanyika vizuri.

Bandika kikaangio jikoni, weka mafuta mengi kiasi, subiri yachemke na tengeneza umbo la mviringo kutoka kwenye nyama, samaki au kuku, kisha chovya kwenye rojo la mkate na mayai.

Tumbukiza mviringo wa mchanganyiko kwenye mafuta, mmoja baada ya mwingine ili kupata matokeo mazuri kwa kutumia kijiko kikubwa chenye madundu ili kuchuja mafuta.

Mchanganyiko wako ukae kwenye mafuta kwa muda wa sekunde tano hadi nane mpaka uwe rangi ya kahawia na hapo utakuwa umeiva vizuri.

Ipua na acha vikauke na tayari msosi wako utakuwa tayari kwa kuliwa. Unaweza kula kama kifungua kichwa au wakati wowote kwa kutumia soda, juisi au maji.

# MAISHA NI NYUMBA

**Na Elizabeth Zaya**

## JINSI YA KUKABILIANA NA NYUFA KWENYE NYUMBA



UZIO ni moja ya sura ambayo unaweza kutumika kama urembo wa nyumba kulingana na namna mhusika anavyotaka uwe kwa kutegemea na bajeti au ubunifu unaotumika kuutengeneza.

Kwa ujumla nyumba inapozungushiwa uzio kwa ajili ya ulinzi, usalama, faragha au mwonekano, lakini unasaidia pia kuongeza thamani ya nyumba.

Kwa mazingira yetu ya Kitanzania kuna uzio wa aina mbalimbali ikiwamo wa matofali, mbao, miti, makuti, chuma, aluminium, wavu na bati.

Mtaalam wa masuala ya ujenzi, Silvester Kambona, anasema yapo mambo ya kuzingatia kabla ya kuweka uzio wa nyumba.

Anasema ni vyema ukaepuka kukurupuka kuchagua uzio kabla hujafahamu gharama za utunzaji wake na endapo utaamua kimakosa, upo uwezekano wa kuharibu mwonekano wa sura ya nyumba yako hata kama ni nzuri kiasi gani.

"Kwa mfano unapoweka uzio wa mbao, unatakiwa ujue kwamba unatakiwa kupakwa rangi mara kwa mara na ujue zinaoza pia baadae, kwa hiyo zinahitaji maboresho ya kila mara kwa sababu bila kukufanya hivyo zinaharibika, hivi ni vitu ambavyo unapaswa kujua katika kila aina ya uzio unaotaka kuweka,"anasema Kambona.

Kabla ya kutengeneza uzio unatakiwa ufahamu uwe kwa mtindo gani.

Anashauri kwamba uzio wa kurembesha zaidi katika lango kuu ikiwamo kuweka taa za rangi unasaidia kuweka mwonekano mzuri wa ukuta na nyumba kwa ujumla.

Kambona anashauri kuweka uzio wenye kuleta faragha na wa kuimarisha ulinzi katika nyumba na siyo bora uzio.

Anasema uzio unaoacha nafasi au matundu katika nyumba hauna faragha na wala hauwezi kukulinda vya kutosha, ila unakupa starehe ya kuangalia kinachoendelea nje ya makazi yako unapokuwa umejipumzisha.

# MPANGILIO

## DONDOO MUHIMU YA NAMNA YA KUCHAGUA MITINDO YA MAUA NJE YA NYUMBA YAKO.

1: Mtindo wa Kirusi, maua upandwa karibu na madirisha, hii humfanya mmiliki au wageni kufurahia rangi nzuri ya maua wakiwa ndani.


2: Mtindo wa Ulaya. Hutumika viwango vikali vya ubunifu, hapa maua na miti hupandwa kwa pamoja na kufanya kama pori nje ya nyumba. Pia barabara nyembamba hujengwa pembeni ya maua, huku nakshi mbalimbali huwekwa kama vitanda, vyungu vyenye maua nk.

3: Mtindo wa Rustic, maua hupanda pamoja na miti ya matunda, aina hii humfanya mtu kupanda maua kila mwaka ili yawe mazuri.

4: Mitindo ya Asia, mara nyingi huwa na mchanganyiko wa maua ya kudumu na yale ya muda mfupi. Maua yenye rangi ya kupendeza hutengenezwa huwekwa kipaumbele zaidi.



# KATUNI


KATUNIKA KI'DOMOKRASIA
BY ABDUL KINGO - 2020
SMS - 0621 412 879
MUUNGWANA LAZIMA AKUBALI KAGALAGAZWA ANAJIFUTA VUMBI' MAISHA YANAENDA
BHANAEEEE... KWANZA KULE KUNA KIPUPWE KIKALI SANA NIMEEPUKANA NA 'NIMONIA'
JUKWAANI
Wote Mmeondoka Lakini Kabaki Huyu Muungwana Nahisi Ndiye Niliyeikuta KURA Yake kwangu AU SIO MZEE?
KINACHONIWEKA NI HIYO SPIKA YANGU MLIYOAZIMA
Kweli Kabithaaaa! thafari Hii Ningeshinda Nilipanga Kila Posho Ningeileta Tugawane LAKINI HAMKUTAKA!
Unamaanisha Ungeacha Kabisa KUTUVURUMISHIA Vumbi Ungepaki Na kutugaia Hela? LABDA SHETANI AFE!
Ndugu Mtaalamu Nitarudisha Vipi Heshima Yangu ILIYOPOTEA?
Kakeshe Bar Kusanya Wapambe Agiza Kwa Fujo Majibu Utayaona
Na hapa Mizimu inataka Uache Laki Saba tu.
Hivi Dada Mbona Kila Nikizitundika Hazikai Kichwani ZINAENDA WAPI?
Nikuitie Fundi Huenda kichwa chako Hakina 'ENKA' Zinadondoka
KAUNTA
Tuvumiliane Safari Ya Miaka Mitano SIO MBALI
Na Migonjwa Inayofumuka Kila Kukicha INANITAZAMA Nakatiza katikati Naelekea Huko?
*KINYUNYIZO CHA LEO...
...DANADANA SIO CHENGA...

HABARI KIMATAIFA

# Rais Donald Trump aashiria kushindwa

**WASHINGTON, Marekani**

RAIS wa Marekani, Donald Trump, kwa mara ya kwanza amezungumzia Ishara ya kukubali kushindwa baada ya uchaguzi wa Novemba 3 mwaka huu.

Joe Biden ambaye ni Rais mteule anaendelea na majukumu yake ya kupanga safu ya viongozi kabla ya kuapishwa mwezi januari mwakani.

Trump, ambaye bado hajakubali kushindwa , kwa mara hatimaye ameashiria uwezekano wa kuwapo kwa utawala mpya mwakani.

Akionekana mtaratibu na mnyonge, wakati alipokuwa akizungumza na kikosi kazi chake cha virusi vya corona Ikulu ya nchi hiyo, kiongozi huyo alisema kuna dalili ya utawala mpya.

'' Kwa lolote litakalotokea siku zijazo, hakuna anayejua utawala gani utakaokuwapo, nadhani muda utaeleza." Aliwaambia wasaidizi wake.

Shinikizo linaendelea kongezeka dhidi ya Trump, kutoka kwa wanachama wenzake wa Republican, akibali kushindwa na kusaidia kurahisisha utamaduni wa kubadilishana uongozi. Matokeo katika jimbo la Georgia na North Carolina yalikuwa ya mwisho kutolewa katika mbio za kuingia Ikulu ya White House.

Hata hivyo, kurudia kuhesabiwa kwa mikono kwa kura kunatarajiwa kufanyika katika jimbo la Georgia, kutokana na wagombea hao kuzidiana kwa idadi ndogo ya kura.

Maofisa wa Biden walisema hawatarajii matokeo kubadilika katika jimbo hilo.

Wakati huo huo , maofisa wa Biden bado hawajapata uwezo wa kupata taarifa za siri za usalama, mashirika ya kitaifa na pesa zinazohitajika kuhakikisha kunakuwepo na urahisi wa kukabidhiana madaraka baina yake na Trump. Msemaji wa Biden Jen Psaki alisema ukosefu wa taarifa hizo unaweza kuathiri uwezo wake wa kuongoza.

"Unahitaji taarifa zilizofika kwa wakati halisi kukabiliana na mzozo wa muda huo ," alisema.

Akiongezea kauli yake kuhusu miito hiyo, mkuu wa zamani wa wafanyakazi wa Trump, John Kelly, alisema kuwa kuchelewa kuanza kwa kipindi cha mpito cha kupokezana madaraka kunaathiri usalama wa taifa. ''Sio mchakato ambao unaanzia kutoka sifuri hadi 1,000 kwa saa''. aliliambia gazeti la Politico.

Katika hatua nyingine, wafanyakazi wa zamani wa usalama waliitaka GSA kumtambua rasmi Biden ili aweze kupata taarifa muhimu kuhusu usalama wa taifa.

**BBC**



Watoto wakicheza kwenye maji baada ya mafuriko kuathiri nyumba za wakazi wa mji wa Bacoor, Jimbo la Cavite, nchini Philippine. **(PICHA: EPA-EFE)**

## Mapigano Tigray yasambaa zaidi

**ADIS ABABA**

ETHIOPIA imesema wanajeshi watiifu kwa chama tawala katika jimbo la Tigray, wamefyatua makombora kuelekea jimbo jirani la Amhara.

Taarifa ya serikali ilisema makombora yalifyatuliwa jana usiku kuelekea miji ya Bahir Dar na Gondar na kusababisha uharibifu viwanja vya ndege.

Chama tawala cha Ukombozi wa Watu wa Tigray (TPLF) kimelaumiwa kwa shambulizi hilo.

Kiongozi wake Debretsion Gebremichael, aliliambia shirika la habari la AFP, kuwa hana taarifa kuhusu mashambulizi hayo, lakini alidokeza kuwa viongozi wa TPLF waliahidi uwanja wowote wa ndege utakaotumiwa kulishambulia jimbo la Tigray , utalengwa na jeshi lao.

Viwanja vya ndege vya Bahir Dar, ambao ndio mji mkuu wa jimbo hilo, na Gondar vinatumiwa na ndege za kijeshi na kiraia

**DW.**

## UN, AU kuondoa walinda amani Darfur

**EWYORK, Marekani**

VIONGOZI wa Umoja wa Afrika, na wa Umoja wa Mataifa wamependekeza kusimamishwa mpango wa askari wa kulinda amani katika jimbo la Darfur.

Uamuzi huo ulitolewa juzi baada ya ya kushuhudiwa mabadiliko makubwa ya kisiasa nchini Sudan.

Katika ripoti yao ya pamoja iliyowasilishwa kwenye Baraza la Usalama, jumuiya hizo mbili zilipendekeza ujumbe wa askari wa kulinda amani ujulikanao kama UNAMID, uondolewe Sudan kuanzia Desemba 31.

Ujumbe wa UNAMID ambao umekuwa ukihudumu tangu 2007, una askari 8,000.

Katibu Mkuu wa Umoja wa Mataifa, Antonio Guterres na Mkuu wa Umoja wa Afrika, Moussa Faki, walikadiria kuuondoa ujumbe huo Darfur, kutachukua miezi sita.

**DW.**

# Pompeo afanya ziara ya kushangaza Ulaya

**PARIS, Ufaransa**

WAZIRI wa Mambo ya Nje wa Marekani, Mike Pompeo, ameanza ziara ya kutembelea nchi saba za Ulaya Mashariki.

Katika ziara hiyo ambayo ilianza jana, nchini Ufaransa itamchukua siku saba kumaliza kabla ya kuelekea mashariki ya kati.

Hata hivyo, ziara ya Pompeo, inaonekana kama kitu kisichokuwa cha kawaida kutokana na nchi zote alizopangiwa kuzitembelea, zimempongeza Joe Biden kwa ushindi wake katika kiti cha urais wa Marekani.

Lengo la ziara hiyo ni kuimarisha na kuunga mkono vipaumbele vya rais anayeondoka madarakani Donald Trump.

Pompeo atakwenda pia Mashariki ya kati, atakakotembelea makazi ya Israel ya walowezi wa kiyahudi katika Ukingo wa Magharibi, kitendo ambacho ni kinyume na mawaziri wengine wa mambo ya nje wa Marekani waliomtangulia waliojiepusha kuyatembelea.

Hata hivyo, hadi sasa mwanadiplomasia huyo wa ngazi ya juu wa Marekani, rais wake na baadhi ya wanachama wa Republican hawajakubaliana na matokeo ya uchaguzi wa Novemba 3, mwaka huu.

Kulingana na Waziri wa Mambo ya Nje wa Ufaransa, Le Drian, Pompeo atakutana pia na Rais Emmanuel Macron siku ya Jumatatu.

Rais huyo wa Ufaransa ambaye alizungumza na Biden siku nne zilizopita na kumpongeza, hakuwa na uhusiano mzuri na Trump.

**DW**

## MAKALA

# Tusikate tamaa



Na Magabilo Masambu

NI wazi kwamba baada ya uchaguzi mkuu uliofanyika Oktoba 28 , lazima maisha yaendelee pamoja na kwamba inawezekana ikatuchukua muda mrefu kabla hatujasahahu kabisa kwasababu inategemea pia mchakato huo umetugusaje kwa maana ya furaha au maumivu kiasi gani tumepitia na hii ni kwasababu kila jambo tufanyalo huwa na matokeo mawili chanya ama hasi, yakiwa chanya huwa tunafurahi na yakiwa hasi tunahuzunika.

Kukata tamaa ni sababu mojawapo na pengine kubwa zaidi iliyoharibu maisha ya wengi, wengine wamepoteza maisha, wamekuwa wagonjwa wa magonjwa yasioeleweka, wengine wamejikuta wakisimama bila kufahamu wafanye nini baada ya kukata tamaa ya maisha, lakini tunapaswa kufahamu kwamba maisha huisha.

Maisha yanafanana kabisa na majira ya mwaka huna haja ya kukata tamaa. Katika mwaka huwa tuna vipindi tofauti, kipindi cha baridi na cha joto, nyakati za mvua ama jua, haya yote Mwenyezi Mungu aliyaweka ili nyakati zote zisiwe zenye huzuni wala zisiwe zenye furaha tu. Maana yake ni kwamba ukicheka leo kuna siku utalia na ukilia leo kuna siku utacheka, ukihuzunika leo siku zenye furaha ziko mbeleni na ukifurahi leo kesho utahuzunika halikadhalika na mengine yote yako hivyo.

Ni muhimu kufahamu kwamba kila jambo lina wakati wake unaweza kutafuta sana, lakini kama wakati haujafika hutafanikiwa, lakini pia ukipata leo kumbuka siku za kupoteza zinakuja mbele yako.

Tofauti hizi zinatufanya binadamu tukamilishe ubinadamu wetu wa kutegemeana wakati wote hivyo ni mwiko kukata tamaa kwasababu hujafanikiwa leo kesho itakuwa zamu yako.Katika maisha tunapishana sana kuna watu waliwahi kupata elimu, lakini baada ya masomo wamechelewa kupata kazi walizozihitaji au wamezikosa kabisa. Wengine wamechelewa kupata elimu wakawahi kupata kazi, wengine wakawahi kuoa ili wapate watoto mapema wamejikuta wanazeeka bila watoto na wengine wakachelewa kuoa au kuolewa wakapata watoto mapema hayo ndiyo maisha.

Katika utafutaji tunapitia mengi, lakini lazima tuwe na matumaini kwamba siku moja tutafanikiwa ni wakati gani hilo analijua Mungu pekee kazi yetu kama binadamu ni kutokata tamaa na kutaka kulazimisha yasiowezekana kwa wakati usiofaa, wengine watauliza wakati unaofaa ni upi? Wakati unaofaa ni ule utakaokuwa umefanikiwa!

Wakati mwingine unakata tamaa ukiwa ukingoni mwa mafanikio na kujikuta mafanikio yakienda kwa mwingine asiyekusudiwa na matokeo yake mafanikio hayo hugeuka na kuwa laana, tuendelee kuwa na matumaini kwamba siku moja tutashinda katika shughuli zetu mbalimbali za kila siku bila kuchoka wala kukata tamaa.

Kwa wataalamu wa masuala ya umeme jina la Thomas Alva Edson sio geni masikioni mwao. Kwa mujibu wa Wikipedia inaonyesha huyu mwamba alifanya majaribio mengi sana katika kuboresha balbu za umeme ambazo leo tunazitumia majumbani mwetu na baada ya kufanya majaribio mara elfu, msaidizi wake alimwambia wamefanya kazi ya bure bila mafanikio, lakini yeye alimjibu kwamba kufanya na kutofanikiwa kumewawezesha kutambua aina za vifaa 2000 ambazo hazikufaa kuboresha balbu! Hapa kuna funzo kubwa kwamba pamoja na kujaribu sana bila mafanikio kumbe mafanikio ni pamoja na kujifunza kitu gani kimekufanya usifanikiwe.

Katika maisha wanaotukatisha tamaa ni watu wa karibu yetu wanaweza kuwa wanafamilia au marafiki wa karibu na wengine wanathubutu kukupatia uzoefu wao katika mambo waliyoshindwa bila kufahamu kwamba wao si wewe na wewe si wao. Si jambo baya kujifunza kwa walioshindwa, lakini uzoefu wao ukupe njia za kutatua changamoto zilizowashinda.

Mafanikio hayawezi kuja bila kujaribu na kushindwa. Dk. Schuller anasema “The failure is not final” akimaanisha kushindwa sio mwisho, hata mtoto mdogo anayeanza kutembea huwa anaanguka mara nyingi zaidi na kusimama tena na mwisho huwa anatembea. Pamoja na kwamba hayo majaribio wakati mwingine yanamsababishia kuumiza mwili.

Mwisho, vipindi vya maisha ni vya mpito hakuna kipindi kitadumu wakati wote kama ni shida au raha zitakuwa za muda tujipe moyo kwamba leo huna kesho utakuwa nacho, leo umeshindwa kesho utashinda kwa kuwa wenye navyo pia upo wakati watavikosa ndivyo maisha yalivyo.

**0689157789**
**magabilomjalifu@gmail.com**

## BURUDANI ILIYOTIKISA ENZI HIZO

# Maisha ya kuombana mboga, chumvi yalivyokuwa



Na Adam Fungamwango

MAMA Tabia, una chumvi kidogo?” ‘Mama Salima, ugali wangu haujakomaa, naomba unga kidogo nikakomazie ugali wangu.” Mwingine atatuma mtoto wake, atakuja na kusema “Mama Juma, mama kanituma mboga, kasema umepika dagaa ama hamu nalo leo.” Mama Juma naye atamjibu “Na yeye si kapika maharage, ukienda mwambie na yeye anichotee kidogo.”

Haya ni maisha ya kawaida kabisa ambayo Watanzania wengi waliishi kwenye miaka ya 1970 hadi 1990 katikati, wakati watu walipoacha sasa kuishi kijamaa kwa vitendo, badala yake kubaki na nadharia zaidi.

Ukisema watu wakati huo walikuwa na roho nzuri si kweli kwa sababu hata leo wapo watu wana roho iliyotakata kweli. Lakini aina ya maisha haya kwa sasa hayapo au yamepungua kwa kiasi kikubwa. Yalikuwa maisha ya kupeana vitu. Mtu aliweza kutoa kitu hata kile kidogo ambacho anacho, anagawana na wenzake.

Kuna mtu aliwahi kuniambia kuwa maisha yale yalianza kupungua pale watu walipoanza kujenga nyumba zao na kuzungushia ukuta wa matofali, badala ya michongoma. Wapo ambao leo wanasema aina ile ya maisha iliwafanya watu wengi kubweteka na kuona maisha ya ni rahisi tu kiasi kwamba baadhi yao walikuwa wavivu na wakashindwa kufanya kazi kwa bidii.

Iwe kweli au si kweli, lakini yalikuwa maisha fulani mazuri ya kusaidiana kwa shida na raha. Yalikuwa maisha ya kijamaa zaidi ambayo yaliwafanya majirani wote kujiona kama ndugu badala ya kila mmoja kujiona bora kuliko mwenzake.

Nazungumzia maisha haya ambayo watu wengi waliishi uswahilini na wakati mwingine nyumba za kota, ziwe na raia wa kawaida, ziwe na maafande, Watanzania wote waliochanganyika walikuwa na mfumo mmoja tu wa maisha.

Hii haihusiani na wale waliokuwa wakiishi sehemu za kitajiri au ‘uzunguni’ kama wenyewe wanavyoita. Maisha ya aina hii yalikuwa nchini nzima, kutokana na kile kilichoitwa ‘Ujamaa na Kujitegemea’.

Haikuwa rahisi rahisi sana familia yoyote kulala na njaa hata kama siku hiyo pesa hakuna. Kama ni mpangaji, basi watoto watakula kwa wapangaji wengine. Na wazazi nao watafanya utaratibu wao wa kupewa chakula au pesa. Huwezi kusikia kesho mtu anatetwa au kusimangwa.

Yalikuwa maisha ya kawaida sana kwa sababu kuna msemo unaosema ‘leo kwangu kesho kwako’. Siku yoyote yanaweza kumtokea mwingine. Lakini pia watu wengi wa zamani walikuwa waadilifu, waliotoka kwenye malezi mema yasiyo ya kudekezwa. Walifundishwa utu, nidhamu na kuheshimu yoyote yule wanayemwona bila kujali alivyo, cheo chake, ukubwa au udogo wake.

Ndiyo maana leo tunashuhudia, mtu anamlipia mtoto wake nauli ya mtu mzima kwenye daladala, halafu anapanda mtu mzee, anasimama wanamwangalia tu. Mtoto aendelea kukaa huku mtu mzima amesimama tu hadi atakapoteremka kisa mama au baba kamlipia mtoto wake.

Zamani huwezi tu kufikiria kitu kama hicho kitatokea. Haiwezekani na haitowezekana mtoto akae kwenye kiti si kwenye daladala au hata nyumbani, halafu mkubwa akiwa amesimama au kukosa kiti. Watoto walifundishwa kuheshimu wakubwa, hivyo kabla hata hajaambiwa, atasimama na kumpisha mkubwa.

Leo hata vijana wa sasa anakaa kwenye siti, wakisikiliza muziki na vidude vyao ya kusikiliza muziki masikioni, basi kama hakuoni vile mzee anahangaika kasimama mbele yake.

Si kwamba kinamama waliokuwa wakipeana mboga, unga, mchele wakati mwingine walikuwa hawana kitu au walikuwa masikini sana, hapana. Au waliokuwa wakitoa ndiyo wana pesa au uwezo, la hasha. Ilikuwa ishara ya ushirikiano, upendo na umoja. Kwa sababu leo anacho huyu, kesho huyu naye atakuwa hana. Au wote wanacho, wanaamua kusambaziana upendo tu.

Unaweza kukuta majirani au wapangaji wakala ugali na mboga saba. Si kama zote wamepika. Mmoja anaweza kupika matembele tu. Akayasambaza kwa wenzake saba kidogo kidogo. Na yeye huko kote akapewa hapa dagaa, hapa nyama, kule maharage, kwingine samaki, kwa yule mlenda na aliyepika samaki akafanya vivyo hivyo kwa wenzake na yeye akapewa mboga kwa wote aliowapa.

Katika jiji la Dar es Salaam kulikuwa na baadhi ya nyumba zinatengeneza siki za mbilimbi. Halafu zinaanikwa juu ya bati. Wakati wa chakula cha mchana, watu wanaongozana kwenye kuomba. Wote wanapata. Hauziwi mtu. Hayo ndiyo yalikuwa maisha ya wakati huo. Ndiyo maana wengi waliyaona kama rahisi hivi. Ilikuwa ni burudani tu.

Kwa sasa hata huko uswahilini watu wanaishi kizungu. Kila mmoja kivyake. Kama huna kitu utalala na njaa. Hakuna kuombana chumvi, kibiriti, mboga wala sukari. Unatakiwa upambane mwenyewe. Kama huna lala. Ukienda kuomba chochote kile, utatangazwa mtaa mzima. Utaonekana mtu wa ajabu. Na si kama hawafanyi hivyo kwa sababu wanajitosheleza, wengine hawana kitu kuliko hata wale wa zamani ila tu maisha yamebadilika. Watu pia wamebadilika.

Kimekuja kizazi fulani hivi cha watu wenye tabia za ubinafsi. Kila mtu na familia yake tu. Hata mwenye uwezo ukimuomba naye atakutangaza tu.

Zamani, watoto waliweza kula nyumba yoyote ile. Na atakayekataa, atakwenda kusemewa kwao kuna ni mchoyo, anakataa kula kwa sababu wenzake wasije kula kwao. Watoto walibadilisha ‘ruti’ za kula. Leo nyumba hii kesho nyingine. Kwa sasa si wengi wenye tabia hiyo. Wakati wa kula mtoto atatimuliwa aende kwao kwanza, wenzake wakila ndiyo arudi. Hapa kuna utata. Ukiuliza kama huo ni uchoyo, utaambiwa hapana.

Wazazi wa zamani walikuwa wavumilivu na wenye busara. Utaambiwa kwa sasa unaweza kumpa chakula mtoto wa watu akapata matatizo ya tumbo, mama yake akaja na nguo mkononi kuwa wanataka kumuulia mwanaye kwa uchawi. Ndiyo maana watoto wa jirani wanatimuliwa kwanza.

Ukifikiri, utaona kuna ukweli ndani yake. Wa zamani wangeshirikiana kumtibia au kumpeleka hospitali kwa sababu wataona ni bahati mbaya. Wa sasa watasema aliyempa chakula ni mchawi. Ndiyo maana tunaona hata watoto wa wazazi wa kisasa wakichapwa na walimu shuleni, wanafunga vibwembwe kwenda kumfungua kazi mwalimu. Lakini watoto wa zamani hawakuthubutu kwenda kwao kusema amepigwa na mwalimu. Kisa, angeulizwa sababu. Halafu ingeweza kumfanya akatandikwa tena nyumbani.

# HADITHI

WASWAHILI wanasema mshika mawili moja humponyoka na karamu mbili zilimshinda fisi. Cecilia, msichana mwenye kila sifa ya kuitwa msichana mrembo, anaangukia kwenye mapenzi ya vijana wawili. Mmoja ni fukara na mwingine mwenye uwezo. Kutokana na mwenyewe kutokuwa na msimamo wenye kueleweka, anawaingiza vijana hao kwenye chuki na visasi, vilivyoambatana na wivu uliopindukia na kusababisha maafa makubwa. Ni kisa cha kusikitisha, kutisha na kuhuzunisha, lakini chenye elimu kubwa.

# Adui Namba Moja-8

**Na Adam Fungamwango (0716 350534)**

NIMEKUELEWA Cecy. Hata mimi nakupenda na nitaendelea kukupenda daima kwa sababu moyo wangu ulikuchagua wewe pekee. Hata hivyo, nilivunjika moyo pale uliponikataa. Halafu si kunikataa tu, lakini ukanikandika na maneno mabaya. Maneno ya kukatisha tamaa.

Unajua yale maneno ni bora uambiwe na mtu mwingine. Lakini siyo unayempenda. Yanauma sana." Mashaka alitoa nyongo.

Sauti aliyokuwa anaongea haikuwa kama mtu anayesimanga au kulaumu. Alikuwa kama analalamika na kuugulia maumivu yaliyo moyoni mwake.

"Jamani Mashaka, najuta, usirudie tena kunikumbusha kilichotokea nyuma."

"Cecy, mimi nakwamba nitaendelea kukupenda. Nimekuelewa ila naomba kwanza nipe wiki moja nitafakari."

"Ina maana bado hujakubali msamaha wangu Mashaka?"

"Hapana, kutafakari maana yake nikae na kumwomba Mungu, ili nikikusamehe kusiingie tena kidudu mtu."

Cecy ikawa inakuja, inakataa. Ni kama alikuwa anataka kumwelewa, lakini baadaye anashindwa kumwelewa. Hata hivyo, aliona heri nusu shari kuliko shari kamili. Hata Mashaka angeamua kukataa, asingeweza kumfanya kitu chochote.

"Mashaka rudisha moyo wako, dada anakupenda sana, na wewe unampenda. Kwenye mapenzi ya kweli changamoto kama hizi ni lazima zitokee." Badaka naye aliingilia.

"Unafikiri dada yako alivyokuwa ananikataa ningetafuta mwanamke mwingine? Ningekuja kukuoa wewe tu mdogo wake, inatosha, wala nisingeenda mbali."

Vilifuatia vicheko kutoka kwa Cecy ambaye alikuwa katika hali ya wasiwasi na kutojiamini muda wote.

"Nyinyi wala msiwe na wasiwasi na mimi, kuweni na amani, kila siku niko na nyinyi. Mungu akipenda yataisha tu haya."

*************************

Kwenye mtaa mmoja, maeneo ya Kinondoni kwa Manyanya, gari moja aina ya Toyota IST rangi nyekundu lilikuwa limepaki pembeni kidogo.

Dereva wa gari alimwita mtoto na kumtuma kwenye nyumba ya tatu kutoka alipopaki.

Ilikuwa majira ya saa 11:00 jioni hivi. Baadhi ya watu walikuwa wakirejea kutoka vibaruani.




**Anajali kila kitu. Anajali hisia za mwenzake. Anamjali kwa shida na raha. Kwenye raha wanakuwa wote na inakuwa raha isiyo kifani. Mwenzake anapokuwa na tatizo au shida, atakuwa naye kwa shida hiyo, kwa kuitatua na hata kama hawezi, basi itakuwa kwa ushauri, mawazo au kuliwaza.**

Dakika tano baadaye, msichana mmoja aliyeonekana mwenye wasiwasi hivi, alitoka akiwa ameongozana na mtoto aliyekwenda kumwita.

Alipoliona gari, alionekana kushtuka kidogo. Miguu yake ni kama iligoma kwenda. Sekunde chache baadaye alionekana kubadili mawazo na kuendelea mbele alikoitwa.

Ni kama alikuwa kichwa chake kilikuwa na watu wawili waliokuwa wakishauriana. Mmoja anasema twende na mwingine akikataa.

Alionekana kutokuwa na raha wala amani. Alikuwa anatembea kama mbuzi aliyekuwa akikokotwa kwenda kuchinjwa.

"Habari yako mpenzi." Sauti ya kukwaruza ilitoka kwa dereva wa gari lile.

Aliyesalimiwa aligundua kuwa haikuwa sauti halisi. Na maneno yale yalificha kitu nyuma yake.

"Nzuri tu, hujambo." Alijibu kwa kujilazimisha.

"Mbona kimya? Siku ya nne leo sikuoni mpenzi wangu, vipi?"

"Naumwa." Alijibu haraka haraka.

"Sasa kama unaumwa unashindwa nini kunipigia simu? Au kuniomba pesa ya matibabu? Si unanipigiana simu mimi kutaka pesa? Sasa imekuwaje?" Hakukuwa na majibu.

"Unasikia Cecy, usinifanye mimi mpumbavu. Au mimi mjinga sana kwamba unaweza kunidangaya. Mimi siyo mtoto mdogo. Kuna kitu unanifanyia."

"Siyo hivyo Zahir, mimi naumwa." alisisitiza.

Wakati huo, Cecy alikuwa ameshika simu yake, akiwa anaichezea. Alikuwa kwenye dirisha la gari la bwana'ake Zahir ambao sasa wako kwenye msuguano mkali.

Ghafla kama kipanga, Zahir alipora simu ya Cecy. Wakati akishtuka na kujiuliza nini kimetokea, tayari Zahir alikuwa ameshafanya alichotaka. Akamrudishia simu yake.

"Sasa tutaona, mimi na wewe nani zaidi. Mimi ni mtoto wa mjini kuliko wewe au huyo kibwengo wako." Alipomaliza kusema hivyo, aliwasha gari na kuondoka, akimwacha Cecy akiwa ameshikwa na bumbuwazi.

Kama alivyofikiria tangu mwanzo ni kwamba Zahir hakuja kwa heri. Alikuja kwa shari. Ila hakutegemea kama anaweza kuondoka pale bila kuchapa walau kofi. Alichoambuliwa ni maneno mabaya.

Hakujua ni kwa nini aliamua kuondoka, mara tu baada ya kumpora simu na baadaye kumrudishia. Hili lilimtisha kidogo Cecy. "Nini amefanya?" Alijiuliza bila majibu.

Mawazo yakamrudisha nyuma kuwa ni wiki na nusu sasa tangu alipotoka nyumbani kwa Mashaka, hana mawasiliano tena na Zahir. Pamoja na kwamba anampigia simu aende kwenye baa fulani au sehemu fulani au kwenye hoteli, lakini hafiki, tofauti na zamani.

Akili ya Cecy iligeuka kabisa na kurudi kwa Mashaka na si Zahir tena. Kwa bahati nzuri baada ya siku tatu, Mashaka alimpigia simu na kumwambia amemsamehe na warudishe mapenzi kama zamani.

Hili ndilo alikuwa analihitaji zaidi Cecy. Penzi halisi. Penzi lisilokuwa na shaka. Penzi linaloonekana kuliko kusikika. Mashaka ni mwanamume anayejua kupenda na kujali.

Anajali kila kitu. Anajali hisia za mwenzake. Anamjali kwa shida na raha. Kwenye raha wanakuwa wote na inakuwa raha isiyo kifani. Mwenzake anapokuwa na tatizo au shida, atakuwa naye kwa shida hiyo, kwa kuitatua na hata kama hawezi, basi itakuwa kwa ushauri, mawazo au kuliwaza.

Mashaka anajali kila mtu anayemzunguka Cecy, kuanzia ndugu zake, wazazi wake, hata ndugu ambayo hajawaona. Alisikia Cecy anamwambia shangazi au mjomba ana matatizo fulani, basi na yeye atakuwa mmoja wa walioyavaa matatizo hayo hadi yaishe. Na atakuwa akimuuliza mara kwa mara. Haya ndiyo maisha yaliyokuwa akiyakosa mtoto wa kike.

***************************

"Haloo, nani mwenzangu?"

"Huna haja ya kunijua kwa sababu mimi siyo mwenzako."

"Unasemaje?"

"Nasema hivi. Wewe si ndiyo Mashaka eee. Basi ninakwambia ukome kutembea na mchumba wangu."

"Mchumba 'ako nani?"

"Unamjua, kwani wewe unatembea na wanawake wengi eee?"

"Unajua sikuelewi."

"Ipo siku na wala si nyingi, utanielewa mimi ni nani. Nakwambia hivi, nataka kufanya kitu ambacho kitakuwa fundisho kwa wote wenye tabia ya kuchukua wanawake za watu kama wewe, mwanga mkubwa wee."

"Unasikia, isije ukawa wewe ndiyo unatembea na mchumba'angu?"

"Mimi nitembee na mchumba'ako?" "Si unamzungumzia Cecy? Au mwingine?"

"We Cecy unamjua vipi?"

"Sikiliza bwana wewe. Cecy ni mpenzi wangu mwaka mmoja sasa. Inaonekana wewe ndiyo umevamia. Sasa nashangaa unanijia juu. Wewe ndiyo unatakiwa kuacha kutembea na mpenzi wangu."

**INAENDELEA JUMAPILI**

## HABARI BURUDANI



## UCHEBE TARATIBU, WAACHE WASEMEE MOYO

ALIYEKUWA mume wa msanii Shilole, mjasiriamali Uchebe ameamua kuwajibu watu wanaoleta maneno kuhusu mpenzi wake mpya, Agness, akisema yeye yupo singo hivyo na hachaguliwi mwanamke.

Akizungumza kwenye kipindi cha Planet Bongo kinachorushwa na East Africa Radio, Uchebe amesema kila mtu aangalie maisha yake na watu wasimjaji sana kwani hata yeye ana utaratibu wake wa kuishi.

"Sipo kwenye ndoa na sasa hivi mimi sio mume wa mtu, nina uwezo wa kutoka na yeyote na kufanya chochote kama mwanamume, na mwanaume lazima amfuate mwanamke ili kujua anataka nini haijalishi awe muislam au mkristo" amesema Uchebe



# NANDY

## ameutendea vyema 2020

NANDY anabaki kuwa mwanamuziki wa kike nchini ambaye ngoma zake zimeangaliwa na watu wengi kuliko wasanii wengine.

Kulingana na mtandao wa You Tube, Nandy ambaye anajuliakana kama 'The African Princess' katika ngoma zake tano alizozitoa mwaka 2020, zaidi ya watu milioni 10 wameziangalia.

Katika orodha hiyo, wimbo wake 'Na Nusu' una watazamaji milioni 2,Acha lizame ina watazamaji milioni 6.4, Dozi ina watazamaji laki saba na 'Do me' aliyofanya na mpenzi wake Billnass ina milioni 1.5.

## Tommy wenzio walisema hivyo, wakalainika

MWANAMUZIKI kutoka lebo ya Kings Music, Tommy Flavour, hatimaye amevunja ukimya na kueleza michoro ya 'tattoo' mwilini mwake auhusiani na mapenzi.

Tommy Flavour amesema hatarajii kuchora tattoo ya mpenzi wake Official Lynn kwa sababu hataki kujutia baadaye pale wanapofikia mwisho.

"Sijawahi kuchora ' tattoo' yenye jina lake wala sura yake na hata yeye hajanichora, 'tattoo' ambazo nipo nazo ni za muda mrefu japo kuchora ni uamuzi wako mwenyewe, unaweza ukachora halafu baadaye ukajuta na mimi sitaki kufikia kwenye hali hiyo, " ameeleza Tommy Flavour

## HABARI MICHEZO




# MBAPPE AJIANDAA KUSAINI MKATABA

**PARIS, Ufaransa**

KYLIAN Mbappe atasaini mkataba mpya na Paris Saint-Germain, lakini kwa sharti moja, kwa mujibu wa Diario AS.

Mbappe kwa muda mrefu amekuwa akihusishwa na uhamisho wa kwenda Real Madrid, huku Liverpool pia nayo ikimtolea macho.

Lakini sasa Mbappe anaweza kukubali kusaini mkataba mpya kwa sharti moja tu la kupunguzwa kwa ada yake ya uhamisho kama timu nyingine itataka kumnunua.

Mbappe alikataa mara tatu ofa za mkataba mpya kwa mabingwa hao wa Ligi Kuu Ufaransa maarufu Ligue 1.

"Sasa anaelekea kusaini mkataba mpya, lakini kwa sharti la kupunguzwa kwa ada katika kipengele cha kumuuza," kilisema chanzo kimoja kikinukuliwa na AS.

Mshindi huyo wa Kombe la Dunia na Ufaransa katika mkataba wake wa sasa kuna kipengele cha kumuuza kwa zaidi ya euro milioni 250 kama klabu yoyote itataka kumsajili.

# NEYMAR ARUDI PSG KUJIUGUZA



**PARIS, Ufaransa**

KLABU ya Paris Saint-Germain imetangaza Neymar atarudi Ufaransa kuendelea kujiuguza majeruhi ya nyonga, huku mchezaji mwenzake Moise Kean ameshaachiwa na Italia.

Neymar aliitwa kikosi cha Brazil katika mechi ya kusaka kufuzu Kombe la Dunia 2022 dhidi ya Venezuela na Uruguay licha ya kukosa mechi tatu za PSG zilizopita.

Hata hivyo, fowadi huyo wa zamani wa Barcelona hatapona kwa wakati kuichezea nchi yake katika mechi za kimataifa mwezi huu, na Brazil haikuwa tayari kuhatarisha afya yake.

PSG ilithibitisha Ijumaa kwamba, Neymar atarudi Ufaransa ili kuendelea kujiuguza zaidi.

Wakati huo huo, Kean tayari amesharudi katika kikosi hicho kutoka nchini Italia baada ya kusumbuliwa na maumivu misuli.

Straika huyo ambaye amefunga mabao matano katika mechi saba tangu kutua hapo kwa mkopo kutoka Everton, atakosa mechi za Italia za Ligi ya Mataifa ya Uefa dhidi ya Poland na Bosnia-Herzegovina.

PSG itarudi dimbani Novemba 20, mwaka huu ikicheza dhidi ya Monaco kwenye Ligi Kuu Ufaransa na siku nne baadae watacheza na RB Leipzig kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya.

# Mourinho afungiwa mechi moja UEFA

**LONDON, England**

KOCHA Mkuu wa Tottenham Hotspur, Jose Mourinho amefungiwa mchezo mmoja na Shirikisho la Umoja wa Vyama vya Soka Ulaya (UEFA), imetangazwa.

Mourinho amefungiwa mchezo huo baada ya Tottenham kuchelewa kuanza mchezo wa Ligi ya Europa waliofungwa 1-0 na Royal Antwerp, Oktoba 29, mwaka huu.

Kocha huyo ndio amegundulika kuwa sababu ya Spurs kuchelewa kuanza mchezo huo katika Uwanja wa Bosuilstadion mjini Antwerp mwezi uliopita.

Hata hivyo, adhabu hiyo atatakiwa kuitumikia ndani ya kipindi cha mwaka mmoja, kuanza tarehe iliyotangazwa, kwa maana atachagua mechi atakayokosa.

Tottenham pia ilipigwa faini ya euro milioni 25,000 kwa kwa kosa hilo.

Spurs inaongoza katika Kundi J katika mashindano hayo ya Europa baada ya kucheza mechi tatu na kupata pointi sita, ikiizidi pointi moja Antwerp na LASK kwa tofauti mbao.



HABARI MICHEZO

# DONDOO ZA SOKA
## MAGAZETI YA ULAYA




# DESCHAMPS: UNITED IMEMWATHIRI POGBA

Kocha huyo wa Ufaransa amesisitiza kiungo wake amekuwa akicheza chini ya kiwango kwa sababu ya...

**PARIS, UFARANSA**

WAKATI mgumu unaomkabili Paul Pogba ndani ya kikosi cha Manchester United, umemwathiri nyota huyo kiakili na nguvu, kwa mujibu wa Kocha Mkuu wa Timu ya Soka ya Ufaransa, Didier Deschamps.

Pogba amekuwa na wakati mgumu wa kuwa kwenye kiwango chake msimu huu, huku akihusishwa na kurudi kwa mabingwa wa Ligi Kuu Italia, Serie A, Juventus na miamba wa La-Liga, Real Madrid.

Nyota huyo wa kimataifa wa Ufaransa, amejikuta akiwa benchi msimu huu pale Old Trafford akiwa ameanza katika mechi nne tu kati ya saba za Ligi Kuu England.

Katika mechi tatu za Ligi ya Mabingwa Ulaya Kocha, Ole Gunnar Solskjaer alimwanzisha mara moja tu Pogba.

Kiungo huyo ametengeneza nafasi mbili kwenye Ligi Kuu England, uhakika wa pasi zake umesimama kwa asilimia 79.9, huku akitengeneza nafasi tatu na pasi za mwisho mbili kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya.

Baada ya kuchapwa na Finland kwenye mchezo wa kirafiki majuzi, Deschamps aliulizwa kuhusu Pogba kuelekea mchezo wa leo Jumapili wa Ligi ya Mataifa ya Uefa dhidi ya Ureno ya Cristiano Ronaldo.

"Hayupo kwenye ubora wake, nilijua hilo kabla," alisema Deschamps akiwaambia waandishi wa habari.

"Mchezo ule dhidi ya Finland alitakiwa kurudisha kiwango chake, na pia kwa Olivier Giroud.

"Nilizungumza nao, walijua namna kati walitakiwa kucheza. Unapoona matokeo kama yale ni ngumu kukumbuka kitu chanya.

"Paul hayupo kwenye ubora wake, nilisema hivyo kabla ya mchezo dhidi ya Finland.

"Kama wachezaji wote ambao wameathirika na hali zilivyo kwenye klabu zao, ndio kitu kilichomwathiri Pogba. Ameathirika kiakili na nguvu."

## KWA UFUPI

**UNITED YAMKANA RONALDO**
MANCHESTER United haijadili kumrudisha mshambuliaji wa Juventus na Timu ya Taifa ya Ureno, Cristiano Ronaldo ambaye ana umri wa miaka 35, katika klabu hiyo. **(Manchester Evening News)**

**SEMEDO ANUKIA LIVERPOOL**
LIVERPOOL ipo tayari kutoa ofa kwa Olympiakos kwa ajili ya mlinzi, Ruben Semedo mwenye umri wa miaka 26 raia wa Ureno, ili kuziba nafasi ya Virgil van Dijk na Joe Gomez ambaye ni majeruhi. **(Sic Noticias, via Express)**

**MADRID YAWEKA DAU**
REAL Madrid inaamini wanauwezo wa kumsajili straika wa Ufaransa, Kylian Mbappe kwa pauni milioni 160, kama nyota huyo mwenye umri wa miaka 21 hatasaini mkataba mpya na Paris St-Germain. **(AS)**

**RAMOS, MADRID KUKUTANA**
RAIS wa Real Madrid, Florentino Perez na nahodha, Sergio Ramos watatangaza kuhusu majaliwa ya nyota huyo mwenye umri wa miaka 34 hapo kesho Jumatatu. **(AS)**

**BOATENG BADO YUPO**
MLINZI wa Bayern Munich, Jerome Boateng mwenye umri wa miaka 32, amebainisha kwamba ameshangazwa na uvumi wa kuondoka klabuni hapo mwishoni mwa msimu huu na kujiunga Tottenham. **(Suddeutsche Zeitung, via Teamtalk)**

**ERIKSEN NJIA MOJA**
KIUNGO wa kimataifa wa Denmark, Christian Eriksen mwenye umri wa miaka 28, amebainisha anaweza kuondoka Inter Milan baada ya kukabiliwa na wakati mgumu wa kupata nafasi ya kucheza kwenye kikosi hicho. **(Star)**

**UNITED YAMTAKA CARMO**
MANCHESTER United inawania kumsajili nyota wa Braga mwenye umri wa miaka 21, David Carmo ambaye ni raia wa Ureno. **(ESPN, via Mail)**

**ANCELOTTI AMWANIA ISCO**
KOCHA wa Everton, Carlo Ancelotti anapanga kumsajili kiungo wa Real Madrid, Isco mwenye umri wa miaka 28 ili kutua Goodison Park. **(Le10 Sport)**

**CARVAJAL KUULA MADRID**
BEKI wa Real Madrid na Timu ya Taifa ya Hispania, Dani Carvajal (28), yuko katika mazungumzo ya kuongeza mkataba mpya na mabosi wa klabu hiyo. **(Marca - in Spanish)**

**GRACIA MAMBO MAGUMU**
MLINZI wa Hispania, Eric Garcia amebakia kimya kuhusu majaliwa yake pale Manchester City, huku uvumi ukimhusisha na mpango wa kurudi Barcelona ambako ndiko alikokulia mlinzi huyo mwenye umri wa miaka 19. **(El Mundo, via Manchester Evening News)**

**JIMENEZ AITAJA UNITED**
STRAIKA wa Wolves na Mexico, Raul Jimenez mwenye umri wa miaka 29, amebainisha kwamba, Manchester United ilikuwa moja ya klabu iliyotaka kumsajili kipindi cha majira ya joto kilishopita. **(TUDN, via Metro)**



# NAMUNGO FC YAITUMIA YANGA KUJIIMARISHA CAF

**Na Saada Akida**

KOCHA Mkuu wa Namungo FC, Thierry Hitimana, amesema atautumia mchezo wa Ligi Kuu Tanzania Bara dhidi ya Yanga kama maandalizi ya kuelekea katika mechi ya mashindano ya kimataifa ya Kombe la Shirikisho Barani Afrika dhidi ya Al Rabita FC kutoka Sudani Kusini.

Namungo itaikaribisha Al Rabita katika mechi ya kwanza ya mashindano hayo Novemba 28, mwaka huu kwenye Uwanja wa Azam Compelx na itawafuata Wasudani hao kwa ajili ya mchezo wa marudiano utakaochezwa kati ya Desemba 4 na 6, mwaka huu.

Akizungumza na gazeti hili jijini Dar es Salaam jana, Hitimana alisema kwa sasa akili na nguvu zao wanazielekeza kuikabili Yanga ambayo itamsaidia kumwonyesha ubora na udhaifu wa kikosi chake.

Hitimana alisema Yanga timu kubwa na yenye wachezaji wazuri, hivyo ana imani kwa uimara wao atapata mazoezi mazuri kabla ya kuanza kupeperusha bendera ya Tanzania Bara kwenye michuano hiyo ya kimataifa.

"Katika mechi yetu dhidi ya Yanga, kuna vitu muhimu ninataangalia, kuna vitu pia ninatafuta ikiwamo pointi tatu muhimu, lakini ni moja ya mechi yetu kubwa ambayo tunatakiwa kuitumikia vizuri kwa ajili ya maandalizi ya kukabiliana na wapinzani wetu kwenye michuano ya CAF,".

"Hatuna hofu dhidi ya Yanga, tunaenda kupambana kutafuta pointi muhimu katika mchezo huo, tumejipanga kuhakikisha wachezaji wangu wanapambana kupata matokeo chanya," alisema Hitimana.

Aliongeza wataingia uwanjani kwa malengo la kupambana kama wanavyofanya kwenye michezo mingine, huku akiwataka wachezaji wake kutobabaisha na majina ya nyota walioko ndani ya kikosi cha Yanga.

Kikosi cha Namungo kutoka Lindi, tayari kipo jijini kuendelea na maandalizi ya kuwavaa Yanga katika mchezo wa raundi ya 10 utakaopigwa Jumapili kwenye Uwanja wa Uhuru.

Katika msimamo wa Ligi Kuu Tanzania Bara, Namungo yenye pointi 14 iko katika nafasi ya tisa wakati Yanga yenye pointi 24 iko katika nafasi ya pili nyuma ya vinara, Azam FC wenye pointi 25.



Mchezaji wa gofu, Ally Mcharo, akijiandaa kupiga mpira katika mashindano ya wazi yanayoendelea kwenye viwanja vya TPC vilivyoko Moshi, Kilimanjaro. Mashindano hayo yanayoshirikisha wachezaji wa ridhaa na kulipwa yanatarajiwa kumalizika leo. **PICHA: MPIGAPICHA WETU.**

# Magoli 161 yapachikwa Ligi Kuu

**Na Adam Fungamwango**

WAKATI Ligi Kuu Tanzania Bara imesimama ili kupisha mechi za kimataifa zilizo kwenye kalenda za FIFA, jumla ya mabao 161 yamefungwa kwenye ligi hiyo ambayo iko katika raundi ya 10.

Kwa mujibu wa takwimu zetu, wakati timu zote zikicheza mechi 10, jumla ya mechi 90 zimeshachezwa, mechi 66 zikiwa zimetoa mshindi na mechi 24 zikiwa sare.

Jumla ya wachezaji 104 ndiyo wamo kwenye orodha ya wachezaji waliofunga idadi hiyo ya mabao ambayo 11 yamepatikana kwa mikwaju ya penalti na matatu yakiwa ya wachezaji kujifunga wenyewe.

Takwimu pia zinaonyesha mechi 40 ni za timu kushinda nyumbani, na kuna idadi ya mechi 26 ambazo timu za Ligi Kuu zimeshinda zikiwa ugenini, sare zikiwa 24 mchanganyiko za nyumbani na ugenini pia.

Kwenye msimamo wafungaji mpaka sasa unaongozwa na wachezaji wawili, mmoja ni Mzimbabwe Prince Dube wa Azam aliyezitingisha nyavu mara sita sawa na Adam Adam wa JKT Tanzania ambaye ni Mtanzania.

Ikumbukwe pia Adam, ndiye mchezaji pekee mpaka sasa ambaye amefanikiwa kufunga 'hat-trick' kwenye Ligi Kuu, akifanya hivyo kwenye mechi kati ya timu yake dhidi ya Mwadui, akiisaidia timu yake kushinda mabao 6-1.

Wanaofuatia ambao wamefunga mabao manne kila mmoja ni Meddie Kagere wa Simba, Obrey Chirwa (Azam FC), Meshack Abraham ( Gwambina FC), Yusuph Mhilu (Kagera Sugar) na Bigirimana Blaise wa Namungo.

Wachezaji watatu ambao wameweka rekodi ya kujifunga ni Adson Katanga wa JKT Tanzania, akiisababishia timu yake kufungwa bao 1-0 na Coastal Union, kipa wa Ihefu, Andrew Kayuni akijifunga, timu yake ikichapwa goli 1-0 na Biashara United, huku Hassan Kapona akijifunga bao moja, timu yake ya Dodoma Jiji, ikikandikwa mabao 3-0 na Azam FC.

## Bodi ya Ligi Z'bar yapata viongozi

**Na Hawa Abdallah, ZANZIBAR**

BOSI wa timu ya Kipanga FC, Kassim Mohamed Abdallah, ameibuka mshindi katika nafasi ya Mwenyekiti wa Bodi ya Ligi Kuu Zanzibar katika uchaguzi wa bodi hiyo uliofanyika jana Visiwani hapa.

Abdallah alishinda nafasi hiyo baada ya kupata kura zote 12 zilizopigwa na wajumbe wa bodi hiyo huku nafasi ya Makamu Mwenyekiti ikienda kwa Shekha Mohamed Ali wa KMKM, ambaye naye alipata kura zote 12.

Nafasi ya Mjumbe wa klabu za Ligi Kuu Zanzibar ilichukuliwa na Mohamed Masoud kutoka katika timu ya Malindi ambaye alipata kura 11.

Akitangaza matokeo ya uchaguzi huo, Mwenyekiti wa Kamati ya Uchaguzi, Fadhili Ramadhani Mberwa, alisema mchakato wa kupata viongozi wa bodi hiyo ulifuata taratibu zote zilizowekwa.

Mberwa alisema uchaguzi huo umefanyika kwa uhuru na haki na wajumbe wote waliokuwa wanastahili kupiga kura kuchagua viongozi wanaowataka walitekeleza majukumu yao.

Kiongozi huyo amewataka viongozi waliochaguliwa kufanya kazi kwa ushirikiano na kwa kufuata katiba na kanuni ya bodi hiyo.

Mwenyekiti mpya wa bodi hiyo, Dk. Mohammed alisema ni jukumu la viongozi wote wa ligi kuhakikisha wanafikia malengo ikiwamo kufanya kazi kwa kushirikiana ili kuubeba mpira wa Zanzibar.

## Kurugenzi kuipa makali Gwambina

**Na Shufaa Lyimo**

TIMU ya Gwambina inatarajia kucheza mchezo wa kirafiki dhidi ya Kurugenzi FC kutoka Simiyu utakaochezwa leo kwa ajili ya kuwaimarisha wachezaji wake wanaoshiriki Ligi Kuu Tanzania Bara.

Kocha Mkuu wa Gwambina FC, Fulgence Novatus, alisema lengo la mchezo huo ni kuwaweka tayari wachezaji wake kuelekea mchezo wa Ligi Kuu Bara dhidi ya JKT Tanzania utakaochezwa Novemba 21, mwaka huu.

"Ninacheza mechi nyingi za kirafiki kwa ajili ya kuwaweka sawa nyota wangu, tunatarajia kukutana na JKT Tanzania ambaye ni moja ya timu imara hapa nchini," alisema Novatus.

Kocha huyo alisema sasa hivi kikosi chake kinafanya mazoezi mara moja kwa siku kutokana na hali ya mvua zinazoendelea kunyesha jijini Mwanza.

Aliongeza kuwa, ameamua kucheza mechi nyingi za kirafiki katika muda huu ambao ligi imesimama ili ziwasaidie wachezaji wake kuwa na kasi.

"Ninaipa umuhimu mkubwa mechi hiyo, JKT ni miongoni mwa timu ambazo zina wachezaji wengi wazuri, kwa sababu hiyo tutaingia kwa tahadhari kubwa, msimu huu hakuna timu ya kubeza, timu zote zimejipanga vizuri ili kushika nafasi za juu katika msimamo," kocha huyo alisema.

Aliwataka mashabiki wao waendelee kuwaunga mkono ili wasishuke daraja na kuwakumbusha ushindani umeongezeka zaidi msimu huu kwenye Ligi Kuu Bara.

# Michezo

Jumapili Novemba 15, 2020
Nipashe



## Deschamps: United imemwathiri Pogba

HABARI UK 22

## Mwakinyo azidi kuing'arisha TZ

**Na Mwandishi Wetu**

HAIKUWA kazi rahisi. Hayo ni maneno ya bondia, Hassan Mwakinyo baada ya kumtwanga kwa TKO mpinzani wake ,Jose Carlos Paz kutoka Argentina na kufanikiwa kuutetea mkanda wa mabara wa uzito wa Super Welter unaotambuliwa na Shirikisho la Ngumi la Dunia la WBF katika pambano lililofanyika kwenye Ukumbi wa Next Door Arena, Oysterbay jijini, Dar es Salaam juzi usiku.

Mwakinyo alifanikiwa kushinda mkanda huo katika raundi ya nne baada ya kumshambulia mpinzani wake kwa ngumi nyingi na mwamuzi, Edward Marshall aliingilia kati kabla ya kumaliza pambano hilo.

Ushindi huo umempa Mwakinyo tiketi ya kuwania mkanda wa dunia wa WBF dhidi ya bondia, Lasha Gurguliani wa Georgia katika pambano litakalofanyika ndani ya miezi mitatu kuanzia sasa, kwa mujibu wa Rais wa WBF, Howard Goldberg aliyekuwapo nchini.

Akizungumza mara baada ya kutangazwa mshindi, Mwakinyo alisema ushindi huo ni zawadi kwa Watanzania wote ambao waliamua kumpa sapoti katika pambano hilo na mengine yaliopita.

"Haikuwa kazi rahisi kushinda, Paz ni bondia mzuri, kama nilivyosema, nafanya mazoezi kutokana na ubora wa mabondia ninao pambana nao. Namshukuru Mungu kuniwezesha kushinda katika pambano hili," alisema Mwakinyo.

Aliongeza ataendelea kufanya mazoezi ili kufanya vyema katika kila pambano atakalopata na kulitangaza vizuri jina la Tanzania.

Katika pambano lingine la utangulizi, bondia Fatuma Zarika wa Kenya alifanikiwa kutwaa ubingwa wa WBF baada ya kushinda kwa pointi dhidi ya Mzimbabwe Patience Mastara huku Mtanzania Zulfa Macho akishinda kwa pointi pia dhidi ya Alice Mbwewe kutoka Zambia wakati Hussein Itaba alitoka sare dhidi ya Mkongomani Alex Kabangu.

Naye Mkurugenzi wa Jackson Group Sport ambao walikuwa waratibu wa pambano hilo, Kelvin Twissa, aliwapongeza mashabiki wa ngumi waliofika katika pambano lao la kwanza la ngumi za kulipwa nchini.

Twissa alisema pambano hilo limefungua njia ya kuandaa mapambano mengine mengi yenye hadhi ya kimataifa na yenye ubora wa hali ya juu.



Bondia Hassan Mwakinyo (kushoto), mara baada ya kufanikiwa kutetea mkanda wa mabara wa uzito wa Super Welter unaotambuliwa na Shirikisho la Ngumi la Kimataifa la WBF. Kulia ni Mkurugenzi wa Kampuni ya Jackson Group Sport, Kelvin Twissa, ambao waliandaa pambano hilo dhidi ya Jose Carlos Paz kutoka Argentina. **PICHA: MTANDAO**

# STARS YAJIPANGA 'KUPINDUA MEZA'

●●●Kocha Ndayiragije afunguka ulikuwa mchezo mgumu kwa pande zote mbili...

**Na Adam Fungamwango**

BAADA ya timu yake kuchapwa bao 1-0, Kocha Mkuu wa Timu ya Taifa (Taifa Stars), Etienne Ndayiragije, amesema kupoteza mechi hiyo dhidi ya Tunisia kulitokana na makosa madogo yaliyofanywa na nyota wake lakini ameahidi kuyarekebisha kabla ya mechi ya marudiano.

Taifa Stars inatarajia kuwakaribisha Waarabu hao wa Tunisia katika mchezo wa marudiano utakaochezwa keshokutwa Jumanne kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa jijini, Dar es Salaam.

Kwa matokeo hayo, Tunisia inaongoza katika Kundi J baada ya kushinda mechi zake tatu ilizocheza na kufikisha pointi tisa ikifuatiwa na Equatorial Guinea, Libya na Tanzania ambazo kila moja ina pointi tatu kibindoni.

Ndayiragije alisema matokeo waliyopata yamekuwa somo kwa kikosi chake ambacho kimejipanga kupambana kwa ajili ya kupata matokeo chanya kwenye mchezo wa marudiano hapa nyumbani.

"Mechi ilikuwa kubwa na ngumu. Wapinzani wetu ni moja kati ya timu kubwa Afrika, wapinzani wetu walijitahidi kutushambulia sana, lakini na sisi tulikaa imara. Hiyo inaonyesha jinsi gani mechi ilivyokuwa ngumu kwa pande zote mbili. Tumefungwa kwa sababu walipata penalti.

Ulikuwa ni mchezo mgumu na wenye ushindani, tunarudi nyumbani, tunaamini tutafanya vizuri na kupata matokeo chanya kwenye mchezo wetu wa marudio," alisema Ndayiragije.

Aliwapongeza wachezaji wake kwa kupambana katika mchezo huo licha ya kushindwa kufikia malengo.

"Timu yangu ilijaribu kupambana, tumepoteza kwa penalti, hii inaonyesha wazi mechi ilikuwa ngumu, tutarekebisha makosa yote, tunarudi nyumbani, nina mechi itakuwa bora zaidi," kocha huyo raia wa Burundi alisema.

Katika mechi nyingine ya kundi hilo iliyochezwa juzi, Equatorial Guinea ikiwa ugenini ilipata ushindi wa mabao 3-2 ambayo yalifufua matumaini ya safari yake ya kusaka tiketi ya kushiriki fainali zijazo za Kombe la Mataifa ya Afrika.

Wakati mechi kati ya Tunisia na Taifa Stars iliyochezwa jijini Tunis juzi usiku ilichezwa bila mashabiki, mchezo wa marudiano utaingiza asilimia 50 ya mashabiki wanaoruhusiwa kuingia uwanjani hapo, kutokana na kujikinga na maambukizi ya COVID-19, yanayosababishwa na virusi vya corona.

9 770856 541002 >

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042